

Kile Kipeo
Jeffersonville, Indiana, USA
Julai 05, 1964

1 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Wakati vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu, na—nashangaa ni wangapi hapa walio na ombi ambalo wangetaka Mungu akumbuke, kwa kuinua tu mikono yenu? Sasa, shikilia ombi lako moyoni mwako sasa tunapoomba.

2 Bwana Yesu, Wewe—ile Chemchemi, Chemchemi isiyoisha ya Uzima, itiririke kwetu leo, Bwana, na utusafishe na kutokuamini kote na dhambi zote, tupate kusimama katika Uwepo Wako sasa, tukijua ya kwamba kuna haja miongoni mwetu, ya kwamba tunajua ya kwamba sisi ni wenye dhambi na si—hatustahili baraka yoyote. Lakini basi tunapowazia juu Yake aliyekuja na kuchukua dhambi zetu! Halafu, wakati Damu Yake iko pale, siyo—siyo sisi katika Uwepo wa Mungu, ni Yeye. Ni sauti yetu tu kupitia Damu Yake. Damu Yake inanena. Ee Mungu, basi isafishe mioyo yetu na dhambi na kutokuamini.

Tupe haja za moyo wetu, kwa kuwa kweli tuna shauku hizi za kukutumikia Wewe. Katika hali hizi za kudhoofika na mateso, na mambo ya ulimwengu ambayo yamewekwa juu yetu wakati mwingine, kutukamilisha; tumeambiwa hivyo. Yeye alisema, "Msione kuwa ni ajabu kwamba majaribu haya huwajia." Yote hutenda kazi tu kwa manufaa yetu na kwa kutukamilisha na kutuleta mpaka mahali hapo. Majangwa haya makuu ya ujuzi, ambapo watu wenye haki wanafinyangwa wakawa watakatifu, tu—tunakushukuru kwa ajili ya matukio haya, Bwana. Tusingekuwa na maana, hatutaki kufanya jambo lo lote kinyume na mapenzi Yako. Lakini tunaomba, Baba, ya kwamba katika hili tutaletwa karibu na Wewe.

Na wakati mizigo ni mizito sana hatuwezi kwenda mbele zaidi, ndipo tunainua mikono yetu na kumlilia Baba yetu. Basi sikia kutoka Mbinguni, Bwana.

Tuponye, tufanye wazima, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Bariki Neno Lako asubuhi ya leo, Bwana. Neno Lako ni Kweli.

3 Nasi tumekusanyika hapa sasa kanisani. Tunamwomba Ndugu Neville, na Ndugu Capps, na Ndugu Collins, na wahudumu wengine wote, na—na wadhamini, mashemasi, na washiriki wote, na wageni malangoni mwetu. Jalia hii iwe ni siku ambayo tutakumbuka kwa muda mrefu, kwa sababu ya Uwepo Wako.

Tuko hapa chini ya matarajio makubwa asubuhi ya leo, Bwana. Niliona kwa muda mfupi tu, tumeitwa pamoja. Tunajisikia ya kwamba ni kwa kusudi fulani. Jalia kusudi Lako litimizwe, Bwana. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, tunapojinyenyekeza. Amina.

4 Ni vizuri sana kuwa hapa na kukusanyika pamoja na kanisa hili lililojaa watu. Sikuwa nikitarajia kuwepo mtu ye yote hapa asubuhi ya leo, kwa sababu sikujua, mimi mwenyewe, nitakuwa hapa.

Tumefika tu kutoka Philadelphia. Na kwa hiyo nikaingia, nikidhani itanibidi kwenda Arizona upesi sana, kwa ajili ya kufanya ibada ya mazishi ya rafiki yangu, Kapteni Jim Moseley, mvulana wa thamani sana, mcha Mungu niliyemwongoza kwa Kristo si muda mrefu uliopita, wale watatu Ndugu wa Moseley. Na mmoja wao akaanguka, naye alikuwa kwenye ndege juzijuzi, naye akafa papo hapo. Alilala motoni kwa masaa kumi kabla hawajamfikia. Kwa hiyo Lee ana umri wa miaka ishirini na minane, mkewe ishirini na sita, na—na kuwaacha watoto watatu wadogo; wa kwanza, ana miaka saba. Inasikitisha sana. Nao ... Walipomwingiza ndani, basi iliwabidi kumzika kesho yake. Kwa hiyo ninaninii tu ... Sikuweza kwenda. Nami niliandika tu, ama kutuma kwa telegramu, yale nitakayosema, ama yale ningalisema kwenye mazishi ya Ndugu Moseley. Baadhi ya mambo haya hatuwezi kuyafahamu, lakini hata hivyo Yeye hufanya kila kitu kitende kazi vizuri tu.

5 Tuko hapa katika kumtumikia Bwana, asubuhi ya leo, tukijua ya kwamba—ya—ya kwamba tunamwamini Mungu, ya kwamba tunaamini ya kwamba Yeye atafanya kila kitu sawa kabisa. Haidhuru ni nini, na jinsi inavyofanya kazi, tunajua haina budi "kufanya kazi kwa manufaa." Yeye aliahidi hilo. Haina budi kuwa hivyo tu. Wakati mwingine hatuwezi kuelewa jambo hilo, inakuwa ngumu sana wakati mwingine, bali hata hivyo tunajua ya kwamba ni Kweli, maana Biblia inasema ni Kweli. Na Biblia, kwetu sisi, ni Mungu katika herufi.

Sasa, hatuna budi kuweka imani yetu mahali fulani. Na kama—kama mimi ama mmoja wetu, maishani, alijaribu kufanikiwa maishani hata akawa, zaidi, milionea mara nyingi...Lakini tutafanyaje na hayo? Hatuna budi kufikia mwisho wa safari, na nini—inatufaa nini basi? Mnaona? Na pesa ni—ni hati, ni kitu cha kubadilishana; lakini hauwezi kuibadilisha kwa Uzima. Ni Mungu tu aliye na Uzima.

6 Kwa hiyo tu—tunatambua ya kwamba tuko hapa katika hali ya kivuli. Na mradi tu kuna kivuli, hapana budi kuwe na kitu halisi. Haiwezekani kuwepo na kivuli pasiwepo kilicho halisi mnaona, kwa maana kivuli hufanyizwa kwa kitu halisi. Kwa mfano kama ulikuwa na negativu ya picha ya kitu fulani. Sharti pawe na kitu mahali fulani ama kugusa, nuru kugusa hiyo lenzi ama hapatakuwepo na—na negativu yo yote. Kwa hiyo tunapona ya kwamba maisha yetu hapa ni kivuli na tukijua kwamba tuko katika mfano wa uhai

fulani mahali fulani, ndipo basi tunajua ya kwamba kuna kitu halisi mahali fulani ambacho hiyo nuru imekigusa, nayo inarudisha mng'ao wake hapa duniani. Na sisi ni uakisi huo tu. Kitu halisi kiko mahali fulani. Kama hilo silo, mimi ndiye mtu aliyedanganywa vibaya sana ulimwenguni; Nimetumia maisha yangu bure. Lakini ninajua, bila shaka yo yote, ya kwamba kiko pale. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu tuko hapa. Mnaona?

7 Ninapowaona ninyi watu mkija humu kutoka kila mahali nchini kwa tangazo la ghafla, na wakati mwingine ni kwa kudhania tu, basi inanifanya nijisikie duni sana ninapokuja katika mkutano kama huu, nikiwazia ya kwamba najua watu hapa wamesafiri kwa mamia ya maili wapate tu kuwa hapa kwa ajili ya dakika chache za ibada, kuketi hapa tu.

Mwanamke fulani alitoa tamshi tu, akaja hivi majuzi na kusema, "Nionyeshe mahali mtu huyo alipotembea, na niruhusu nitembee nyuma yake, juu ya ardhi," kasema, "nitapona." Sasa, watu wanakuamini hivyo, nawe ni mwakilishi wa Kristo, basi tufanyeje? Inatupasa kuwa waangalifu sana, kwa maana wewe hujiangamizi tu kwa makosa, unawaangamiza wengine wanaokufuata.

Kwa hiyo, sijui dhehebu wala cho chote cha kuwapeleka. Kuna kitu kimoja tu nilicho na imani nacho. Kama mnaniamini, fuateni yale ninayowaambia. Kwa sababu, ninaamini Biblia, hilo ni Neno la Mungu. Mambo mengine yanashindwa. Mimi ninaninii tu ... Yeye ni Uzima. Yeye ni Neno.

8 Sasa, ninajua ya kwamba ninyi ... Ninapokuja hapa, ninawaweka muda mrefu. Nilimwomba Mungu, wakati nilipojisikia kama nilitaka kuja hapa leo. Nimekuwa na mahojiano na simu nyingi sana, na kadhalika. Ilinibidi kukutana na baadhi yao asubuhi ya leo. Nami nikasema, "Vema, Ndugu Neville bila shaka ananiomba nizungumze." Hiyo ilikuwa Ijumaa. Nami nikasema, "Ndugu Neville labda ataniomba nizungumze. Na ninapofanya hivyo, ndipo ninaomba, Mungu ..." Kuna joto sana, kumekuwa na joto sana. Na Yeye amekuwa mwema akatutumia mvua na kukatiza joto lililozidi sana na kutupa asubuhi njema asubuhi hii. Naomba ya kwamba wema Wake utamtirikia kila mmoja wenu hata mtakumbuka daima kuwa mlikuwa hapa asubuhi hii. Jalia neema Yake na baraka ziwe juu yako!

9 Jana usiku nilimtembelea rafiki yangu aliye mgonjwa, Ndugu Bill Dauch. Simwoni hapa asubuhi ya leo. Kwa namna fulani, sijui. Loo, huyu hapa. Yeye ni ... Naam. Nami nilikuwa nikiwazia: "Mzee wa miaka tisini na mmoja na angali anatembea kishujaa humu—humu nchini, kuvuka majangwa, na kuvuka milima yenye theluji, na barabara zenye kuteleza. Si lazima afanye hivyo. Mungu amekuwa mwema kwake; si lazima afanye hivyo. Angekaa nyumbani na watumishi wampepee kama angalitaka, kama angetaka." Lakini, jambo fulani lilimpata Bill Dauch, alizaliwa mara ya pili. Na hilo lilipotukia, kitu fulani kikaingia moyoni mwake, hata ikawa kusudi lake la kuishi ni kuhudhuria ibada hizi. Halafu basi kama ningekuwa msemaji wa Mungu, je! Ningemdanganya rafiki? Afadhali nife. Basi hebu nimwambie hasa yaliyo Kweli kutoka Biblia hii. Halafu, hilo ni Neno la Mungu. Ninarudia tu yale aliyosema.

Sasa nataka kusoma kidogo kutoka kwenye Biblia.

10 Kabla hatujasoma, ningetaka ku—kusema ya kwamba ninaamini usiku wa leo ni usiku wa ushirika. Nanyi mliopo hapa ... Bila shaka, hao watu wengine labda watarudi makwao, maana hawana budi kwenda kazini. Ninyi mlio hapa katika kusanyiko, kumbukeni, ndugu watakuwa wakifanya ushirika usiku wa leo.

11 Sasa, ninangojea wito wa mwisho kwa Afrika. Hawangeweza, hawakuniruhusu niingie kama mmishenari. Kwa hiyo njia pekee ninayoweza kuingia, chini ... Ninaenda Kenya, Uganda, na—na Tanganyika. Na njia pekee ninayoweza kuingia ... Kwanza, makanisa hayatakuruhusu uingie, maana yananitaka nihubiri jambo fulani upande *huu* na upande *ule*, huko Afrika. Wala sitaingia namna hiyo. Nisingekuwa mnafiki vya kutosha kufanya hivyo. Kwa hiyo ama ninawaambia, "La, bwana, nitahubiri tu yale Mungu anayoweza moyoni mwangu, na hivyo tu." Mnaona? Nami nina hakika haitakuwa yale wanajaribu kunifanya niwafundishe. Kwa hiyo, ubatizo wa utatu, na kadhalika namna hiyo, na kuzozana nao. La.

12 Lakini nimeombwa kwenye mkutano mkubwa, na Ndugu Boze. Yeye yuko tu karibu kuingia kuona mwangaza wa mchana wa yale tunayoamini. Na kwa hiyo nimeomba niingie kama kwamba nilikuwa nikienda kuwinda. Kama wakiniacha niingie, kama kwenda kuwinda ... Kama nikimpata mtu kusema wangenipeleka nikawinde, ndipo nitakapoingia kule, daktari—daktari aliyeko kwenye ubalozi, ni rafiki yangu kutoka Chicago. Na mara nikiingia mle, yeye anasema, "Vema, huyu hapa Ndugu Branham hapa. Hebu na tufanye mkutano." Kwa hiyo, baada ya mimi kuwa kule, ubalozi hauwezi kunikataza. Kama wao ... Kwa hiyo wanajaribu kulifanyia kazi sasa. Kwa hiyo ninatumaini ya kwamba ... Kama ni mapenzi ya Mungu, itatendeka namna hiyo. Mnaona? I—imewekwa tu Kwake. Kama sivyo, basi nitawaarifu. Sitaninii ...

13 Kama ni mapenzi ya Mungu, basi, ninataka kuzungumza juu ya zile Baragumu Saba. Na hiyo itakuwa kama ibada ya siku nane, na hatutakuwa hapa maskanini, labda. Tunajaribu kupata ukumbi hapa.

Sasa sikufikiria kamwe, juu ya ukumbi huu mpya uliojengwa tu hapa juu, ni mahali hasa ambapo nilimwona Yesu mara ya kwanza katika ono. Sasa umejengwa, ukumbi wa mikutano umejengwa juu ya

mahali pale pale. Nilienda moja kwa moja pale hivi majuzi, kuangalia. Nilipotazama na kumwona akiangalia upande wa mashariki, mnakumbuka mkinisikia nikisimulia, nilipokuwa huko nje nikimwombea baba yangu; m—mvulana mdogo, mhubiri mvulana tu. Hapo ndipo nilipomwona. Amepiga hatua, nikimtazama Yeye; Kichwa Chake kiliangalia kando ya pale nilipokuwa. Niliendelea kutembea, nikikohoa, katika uwanja wa majani. Nami nikaendelea kuangalia, Naye kamwe hakugeuka. Ndipo nikaliita Jina Lake, "Yesu." Naye akageuka, akainua mikono Yake, na hayo tu ndiyo niliyokumbuka mpaka mapambazuko. Ndipo nikatoka huko uwanjani, karibu mapambazuko.

Kwa hiyo labda Bwana ataniruhusu nihubiri hizo Baragumu pale. Popote pale, mapenzi ya Mungu yatimizwe.

14 Fungueni Biblia zenu sasa, kwenye Isaya sura ya hamsini- ... ya 53 ya Isaya.

Sasa, tunatumaini ya kwamba Mungu atabariki jitihada zetu dhaifu za kukusanyika pamoja asubuhi ya leo. Tumetoka Philadelphia hivi punde, ambako nilikuwa kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara Wakristo wa Injili Yote, na katika kusikiliza shuhuda zao mbalimbali na kadhalika huko juu.

Ndipo mimi, nilipokuwa nikishuka kwenda, nilikuwa ... Mimi na Billy Paul, na Rebeka na msichana mdogo wa Collins, maskini Betty Collins. Naye Billy anapenda kulala sana, na Becky ni zaidi, na kwa hiyo mimi ... Mimi na Betty tulizungumza. Naye alikuwa ameketi nyuma na Becky, kwenye kiti cha nyuma. Nami nikaona jambo fulani barabarani, likitukia; na, nilipofanya hivyo, kitu fulani kikanijia. Na Betty, kama yuko hapa, aliona niliacha kuzungumza na kuanza kuandika kitu fulani. Hapo ndipo nilipopata somo hili la asubuhi ya leo.

15 Sasa hebu na tusimame kwa miguu yetu. Kama sisi ... Sasa tunasimama kwa heshima ya Neno la Mungu, ninaposoma Isaya sura ya 53.

Ni nani aliyeamini habari zetu? Na mkono wa BWANA amefunuliwa nani?

Angalia, kwanza, ni swali.

Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, Na kama mzizi katika ... nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri; Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.

Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ... ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.

Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa.

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.

Alionewa, lakini ... alinyenyekea, Wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo ... anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake.

Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayesimulia? maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.

Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya, na pamoja na matajiri katika kufa kwake; iIngawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

Lakini BWANA aliridhika kumchubua; Yeye ... amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake.

Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika: kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki... naye atayachukua maovu yao.

Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye ... atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na hao wakosao; walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji.

16 Baba Mungu, Neno Lako ni Taa, Nuru inayoangazia njia ya kila mwamini kuingia katika Uwepo wa Mungu, kwa kuwa inatubeba kama taa mkononi mwetu. Haujatao ya kutosha tupate kuona mwisho tangu mwanzo, na, ila mimi hutembea kwa imani. Lakini kama mtu anavyotembea katika msitu wenye giza usiku

na hapo ndipo tulipo; taa anayoishikilia humwongoza tu hatua kwa hatua. Lakini njia, ingawa inaongoza kwenda juu, tembea tu na Nuru. Na jalia Nuru iangaze leo juu ya Neno, kutuongoza hatua moja mbele kwenye Ufalme wa Mungu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

17 Somo ninalojisikia kuliambia kusanyiko leo ni: *Kile Kipeo*.

Laweza kuonekana jambo la kushangaza kutilia maanani kusomwa kwa—kwa Andiko kama hili la—la mojawapo ya matukio ya Biblia ya machubuko sana na ya mauaji sana, ambapo Biblia inasema kwamba, “Huyu mtumishi Mkamilifu aliyeteswa, na akachubuliwa na kuraruliwa, na hata hivyo kutoa somo hapo kama Kipeo. Ajabu sana. Lakini mimi nina ...

Akili yangu inafikiria, asubuhi ya leo, tunaposafiri kurudi, ninafanya hivyo, kwa miaka michache. Nilikaribishwa huko Forest Lawn, huko—huko California, juu ya Los Angeles. Kusudi langu la kwanza la kwenda kule lilikuwa kutembelea kaburi la—la Aimee Semple McPherson, mwanzilishi wa vuguvugu la Foursquare. Ndipo nikaenda kwenye kaburi lake—lake. Nami...Ingawa si—sikubaliani na mwanamke huyo kama mhudumu, hata hivyo moyoni mwangu, ninampenda na kumheshimu kwa—kwa ajili ya yale aliyoshindania katika ile—ile saa na mateso na mambo aliyopitia katika wakati wake hapa duniani. Na halafu kwa mwanawe—mwanawe mpendwa, ambaye ni rafiki yangu msiri, Rolf McPherson.

18 Na kundi la wahudumu, tulienda kule. Nao ... hatukuwa na wakati wa kuingia kwenye—kwenye ... mahali pa—mahali ambapo wanaiteketeza maiti, na kuiweka ile—ile miili katika sa—sanduku dogo kwenye ukuta.

Na huko wana vitu vya maana sana, kama ile Meza ya Bwana ya Mwisho. Na inaangazwa na nuru halisi ya jua. Nao wana—wana dirisha linalowapa... Wanapoingia, ni nuru; na halafu wa—wanapoanza kuzungumza, inakuwa giza. Na baada ya kitambo kidogo inakuwa giza, ndipo watu wanaondoka. Nao wana hiyo Meza ya Bwana.

19 Na yule mwanamke aliyekuwa na hiyo siri ya jinsi ya kufua kioo hiki kukiingiza mahali hapa, hata, kuchora hizi picha, kumbe, ili—ilipitia katika ukoo mmoja tangu miaka mingi iliyopita. Na sanaa hiyo ilitolewa tu kwa watoto, na wa mwisho alikuwa ni mwanamke. Nao walikuwa wakitengeneza picha hii. Nao walipoanza kukifinyanga na kukichoma moto kile—kile kioo, kukikausha, cha Yuda Iskariote, kikapasuka. Kwa hiyo basi wakajaribu tena, na kikapasuka tena. Naye akasema, “Labda Bwana wetu hataki picha ya adui Wake kando Yake.” Kisha akasema, “Kama kikipasuka tena, hatutaimaliza picha.” Lakini hakikupasuka wakati huo. Halafu, bila shaka, hilo lilikuwa ni jambo la kushangaza, na jinsi ambavyo mambo kama hayo yangetukia.

20 Lakini basi, moja ya mambo muhimu yanayonivutia katika Forest Lawn ni ile ya Michelangelo, ile sanamu kubwa, ile—ile sanamu ya Musa. Hiyo ni—ni nakala yake, bila shaka. Si ile ya kwanza, lakini ilikuwa ni—ni kipeo kikuu. Na niliposimama na kuiangalia, ni—niliipenda hiyo, kitu kinachoonekana kana kwamba (inawakilisha) kina kitu fulani kwake.

Ninapenda sanaa, vizuri sana. Ninaamini Mungu yuko katika sanaa. Ninaamini Mungu yuko katika muziki. Ninaamini Mungu yuko katika maumbile. Mungu yuko kila mahali. Na cho chote kilicho kinyume cha asili ni upotovu. Mungu yuko katika dansi; si aina ya dansi mnayofanya hapa. Lakini wakati wana na binti za Mungu wanapokuwa katika Roho wa Mungu, mnaona, huko ni kucheza. Lakini kama ilivyotulazimu kushindana nayo hata saa 8 usiku wa kuamkia leo juu kule njiani, hiyo ndiyo upotovu wake.

21 Lakini hiki, kile kipeo ambacho Michelangelo alikuwa—alikuwa ametengeneza, ili—ilimgharimu kitu fulani kufanya hivyo. Yeye alikuwa mtu mashuhuri, na iligharimu sehemu kubwa ya maisha yake, kwa sababu alikuwa akichonga kwa miaka mingi sana. Chukua tu mwamba na wa—wa marumaru, na uendelee kuuchonga. Na, mnaona, mtu huyo tu, yule mchongaji mwenyewe, ndiye aliye na wazo akilini mwake la kile anachotaribu kufanya. Yeye, yeye ndiye pekee. Waweza kumwendea na kumwambia, “Kwa nini unachonga-chonga huo mwamba?” Kwa mtu wa nje, ambaye hajui yaliyo moyoni mwake, ni upuuzi. Lakini kwa mtu huyo, yule mchongaji mwenyewe, yeye—yeye ana ma—maono mawazoni mwake, kile anachotaribu kufanya, naye anajaribu kuzaa tena yale aliyokuwa nayo mawazoni mwake katika umbo la—la mnara. Hiyo ndiyo sababu anaichimba kutoka kwenye miamba.

22 Na kufanya hivi, sharti uanzie mwanzoni, na sharti ufuata kielelezo. Mnaona? Huwezi kuchukua kipande kidogo kuanza: “Tutaitengeneza hivi; la, naamini...” La, hana budi kuwa na kielelezo halisi. Na akilini mwake ana kielelezo hicho. Naye hawezi kubadili kielelezo hicho. Sasa, ili kufanya hivi ilimpasa kuchora akilini mwake, kwa sababu hatuna picha halisi za Musa, bali ilimpasa kupata taswira akilini mwake ya jinsi Musa alivyokuwa hasa.

23 Sasa, mchongaji halisi amevuviwa, kama mshairi halisi, ama mwimbaji yeyote halisi, mwanamuziki, ye yote yule. Yote halisi hayana budi kuja kwa uvuvio. Michelangelo lazima awe alikuwa na uvuvio wa vile Musa alivyoonekana kweli. Naye akashika akilini mwake jinsi Musa alivyokuwa. Kwa hiyo akaanza kazi kwa

kipande hiki kikubwa cha marmar kukikata kulingana na ule mfano, na kukichonga, kukisugua, hata akafikia ile picha halisi ya kile kilipaswa kuwa akilini mwake.

24 Kisha alipoikamilisha yote, kila kona imenyoshwa, na kila mahali pamesuguliwa, na macho sawa kabisa, na kila unywele na ndevu, zote jinsi zilivyokuwa, alisimama kando akaiangalia. Na—nawazia ile—ile miaka mingi, mingi sana ya kazi ngumu, na jinsi ilimpasa kushikilia picha ile wakati wote akilini mwake ya yale angefanya. Na hebu wazia tu, ono hilo moyoni mwake kwa miaka mingi sana, kulifanya lionekane hasa jinsi lilivyokuwa! Alishika lile ono kwanza, na jinsi ilivyompasa kulifanyia kazi lile ono, akilikata na kuchonga! Na alipoikamilisha kabisa, hata ikawa kamili hasa, alisimama akaiangalia alipoimaliza asubuhi hiyo, huku ameshika nyundo.

Naye alivuviwa sana alipoiangalia, kwa kuwa picha ya moyo wake ilikuwa imesimama mbele yake, ikiwa katika hali halisi. Kile alichokuwa ameona na yale ... mawazo yake juu ya sura ya Musa, kilikuwa kimesimama mbele yake, kile alichokuwa nacho moyoni mwake miaka hii yote Na kazi ngumu, na masaa kadha ya huzuni, na dhiki, na watoa lawama, na kila kitu, lakini hata hivyo yeye alidumu tu na lile ono hata lilipotimizwa.

25 Na wakati ilipokwisha timizwa, alisimama kando huku ameshika nyundo (nyundo ya mchoraji) mkononi mwake, naye akaiangalia hiyo sanamu. Na uvuvio wa ile taswira, ambayo alikuwa ameiona ya jinsi ya kutenda hayo, ukamvuvia sana hata yeye ... Uvuvio ulimghusa sana hata hakuweza kujizuia na akaipiga gotini na kusema, "Nena!"

Na sasa kuna waa katika hiyo sanamu mashuhuri, gotini, kwenye goti la kuume. Mahali hapo ni yapata inchi sita, juu kidogo ya goti, (niliingiza mkono wangu pale) kina chake *hivi*.

26 Baada ya kutumia wakati huo wote, kwa miaka kadha wa kadha kuitengeneza hii, halafu kwa—kwa ushawishi wa kuona kile alichokuwa ameona moyoni mwake na katika ile picha kimetimizwa, na alichotaka sana kuona, kimekamilishwa Na wakati kilipokamilishwa, alivuviwa sana nayo hata akafikiri kipeo chake kinapaswa kumzungumzia. Naye akakipiga mguuni na kupaza sauti, "Nena!" Nayo ikapata waa. Hiyo sanamu ikapata waa.

Kwangu mimi, hilo waa ndilo lililofanya kuwa kipeo. Sasa, labda kwa—kwa akili inayoweza kuwazia vinginevyo, unafikiri hilo liliharibu. La, kwangu mimi li—lililifanya jinsi ilivyokuwa. Ni—ni ... Kwa maana baada ya miaka mingi sana ya kazi ya ustadi, uchovu, na uvuvio, na kadhalika katika kuitengeneza, jitihada zake zilikuwa zimethibitisha hazikuwa za bure. Ilikuwa ni kamilifu, na hiyo ndiyo sababu akalia, "Nena!" Kwa sababu, alikuwa ameona mbele yake ya kwamba yeye (alikuwa) ameweza kufanikisha, kutimiza maono yaliyokuwa akilini mwake. Na kwa hiyo, chini ya uvuvio, alifanya jambo fulani nje ya sababu, nje ya kawaida. Akaipiga, na kupiga makelele, "Nena!" Mnaona, asingefanya jambo hilo kama angelifikiria. Lakini yeye hakufikiri. Ilikuwa ni uvuvio wa kuona yale aliyokuwa nayo akilini mwake yakiketi pale mbele yake kikamilifu.

27 Jitihada zake, na uchovu wake, kazi za usiku, na kutengwa na ulimwengu kwa siku kadha, na labda anakula sambusa moja. Na—na kuisugua, kisha anarudi na, "Sasa, hivyo sivyo ilivyokuwa. Sasa, haina budi kuwa *hivi*," na kuisugua Ndipo wakati alipoona jambo hilo, kamilifu kabisa, basi aliona katika hali halisi. Ile negatifu ya kile kilichokuwa akilini mwake kilikuwa kimekuwa halisi; kikawa kitu dhahiri; kwa hiyo, kikamjia ghafla. Na ilikuwa halisi sana hata hana budi kupaza sauti, "Nena!"

Kwangu mimi ilikuwa kurudishwa kwa sura. Ilikuwa—ilikuwa ni sifa ya kazi yake, kwamba kazi yake ilimvuvia sana hata hakuweza kujizuia kuipiga na kusema, "Nena!"

28 Nilisimama hapo nikaangalia sanamu hiyo. Nikawazia juu ya masaa ambayo mtu huyo alikuwa hana budi aliyatumia katika kuitengeneza. Walisema ilikuwa ni miaka mingapi. Lakini ilikuwa—ilikuwa kurudishwa kwa sura iliyokuwa akilini mwake, kwa sababu ilikuwa msaada kwa—kwa sanaa yake mashuhuri, kazi yake kuu aliyokuwa akifanya. Na hatimaye alipofaulu, ilikuwa kazi kubwa sana.

29 Sasa hebu na tufungue ukurasa huu, wa Michelangelo, na kukifunga kile kitabu.

Na hebu tufungue Kitabu kingine na kusoma juu ya yule Mchongaji mkuu, Mwenyezi. Ambaye, kabla hakujakuwako na ulimwengu, na kabla misingi haijawekwa, Yeye alikuwa na kile alichotaka moyoni Mwake, Naye alitaka kumfanya mtu kwa mfano Wake. Yeye alitaka kufanya kitu fulani katika—katika uhalisi wa kile kilichokuwa ono Kwake, kile kilichokuwa katika mawazo Yake.

30 Sasa, kwa Michelangelo, hiyo ilikuwa ni sifa ya wazo lake.

Naye Mungu alitaka kumfanya mtu kulingana na sura Yake, yule Mchongaji mashuhuri, Naye akaenda kumfanyia kazi. Nasi tunaona wakati alipoleta vifaa. Ya kwanza labda ilikuwa ni samaki, halafu ndege, na —na halafu vitu vitambaavyo juu ya nchi, na—na vitu vingi ambavyo Yeye alileta. Lakini hatimaye alipokuwa akiatamia, akiwa Muumba, Yeye alikuwa... Yeye hakuwa kama mwanadamu, sasa, mchonga sanamu ambaye hana budi kuchukua kitu ambacho kimeumbwa, kuchonga sanamu. Yeye alikuwa

Mchongaji wa vitu vya Milele. Yeye alikuwa Mchongaji ambaye angeweza kuumba na kukifanya kiwepo kitu kile alichokusudia mawazoni Mwake kufanya. Ama, vinginevyo, Yeye anaweza kufanya kitu kionekane ambacho sifa Zake zilikitaka.

31 Na wakati alipoanza kufanya kazi ya vitu vitambaavyo, kama vile wale—wale—wanyama wadogo juu ya nchi. Halafu, Yeye akaanza kukifanya kutoka hicho hadi kitu kingine, cha hali ya juu zaidi. Hatimaye Yeye akawaumba wanyama wakubwa kama simba, chui mkubwa, dubu. Kisha akawaleta hata katika—katika—katika maisha labda ya—ya nyani, na sokwe, na kadhalika. Sasa, si mabadiliko ya viumbe, kama tunavyofikiria ya kwamba mtu alitoka kwa... Huo ulikuwa ni uumbaji mkamilifu; Mungu akitenda kazi katika mfano.

Lakini hatimaye kulitokea juu ya nchi, ukamilifu, na huo ulikuwa mwanadamu. Na ndipo Yeye angeweza kuona katika mtu huyo, ya kwamba ilionekana kama Yeye. Hivyo sasa, wakati Yeye alipomtazama Huyo, alikuwa kurundishwa kwa sura ya jinsi Muumba wake alivyokuwa. Mungu sasa alikuwa ameweza kufanikisha jambo alilotaka, mtu kwa mfano Wake.

32 Halafu basi huenda nikasema, kwa hili, kwamba, wakati alipomfanya mtu huyu, kulikuwa na kitu fulani juu yake bado ambacho hakikuonekana sawa, kwa sababu yeye—yeye alikuwa peke yake. Na hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa, kwa nafsi Yake; Yeye alikuwa wa Milele. Na mtu sasa, katika mfano wa Mungu, pia aliishi duniani peke yake. Kwa hiyo hapana budi alipiga pigo kidogo upande wake wa kushoto, na kutoka hapo akachukua kile kipande kilichotoka humo na kumfanya msaidizi, mke, basi hakuwa peke yake. Alikuwa—alikuwa, alikuwa na mtu fulani pamoja naye. Na hiyo ndiyo kazi Yake kuu.

33 Na, Yeye, kama mchongaji yeyote mashuhuri angechukua kipeo chake—chake—chake ...

Sasa, kwanza, Yeye alikuwa na kipeo Chake Mwenyewe. Lakini sasa Yeye aliona ya kwamba kile kipeo kilikuwa kipweke, kama alivyokuwa, kwa hiyo akakigawanya kipeo kwa kukipiga ubavuni na akaleta msaidizi.

Na sasa, kuwafanya hao wawili kuwa mmoja, Yeye aliwaweka, kama mchongaji yeyote mashuhuri, mahali ambapo—ambapo ni pazuri. M—mchonga sanamu asingeweza kufanya kipeo kikuu, kisha akichukue na kukiweka kwenye uchochoro mahali fulani, ama kukificha nyuma ya majengo. Kama vile Bwana wetu alivyotuambia, "Mtu hawashi mshumaa na kuuweka chini ya pishi." Tunapofanyika vipeo vya Mungu, hatupaswi kujificha vichochoroni mahali fulani. Sisi—sisi hatuna budi kutoa nuru.

34 Kwa hiyo tunaona ya kwamba—ya kwamba Yeye, baada ya Yeye kutengeneza hiki kipeo, alikiweka hapa juu ya nchi, na kukiweka mahali pazuri sana, katika bustani ya Edeni. Yeye aliweka kipeo Chake, hao wawili wakiwa mmoja, katika bustani ya Edeni. Jinsi ambavyo hapana budi ilimpendeza Yeye, kwamba aliona kipeo hiki kilikuwa kizuri. Yeye, baada ya hayo, tunaona ya kwamba Yeye alipumzika; Alifurahishwa sana na kazi Yake.

35 Sasa kumbukeni, ya kwamba kwa maoni yangu kile kipeo ni lile pigo lililokitia waa kipeo cha Musa katika ile sanamu iliyochongwa na San Angelo.

Na lilikuwa pigo lililoukata ubavu wa kipeo Chake likamtoa bibi-arusi. Na sasa tunawaona kama jamaa kipeo katika bustani ya Edeni. Kilikuwa kizuri sana! Na jambo hilo lilimpendeza sana, mpaka Yeye—Yeye akapumzika basi. Akasema, "Mimi, nitapumzika."

Lakini wakati alipokuwa akipumzika na kuamini kipeo Chake, adui Wake aliingia na akakipata kipeo hiki kikuu. Naye, kwa udanganyifu akatambaa chini ya—ya kuta za ile bustani, kisha aka—akakiharibu hiki kipeo kizuri. Yeye—yeye alikiharibu, hata ki—kikaanguka.

36 Sasa ninajaribu kuangalia hiyo saa. Nami nikamwomba Mike, mpwa wangu, kupiga kengele hiyo katika dakika thelathini, lakini mimi ... Yeye hajafanya jambo hilo, nami tayari nimekuwa na dakika thelathini. Lakini, ni, tunaendelea kidogo. Mnaona? Sasa, sitaki ku—kuvunja sheria hizi. Ni—nilitunga sheria hizi, mnaona, na mimi—mimi ... na hapa ni kuvunja kanuni zenu wenyewe.

37 Sasa angalia, basi, kipeo hiki. Wakati Shetani alipokishika, yule mdanganyifu, alipopenya kati ya zile kuta, na—na kukiharibu hiki kipeo. Kwa sababu jinsi alivyokitengene, nini ... Namna alivyofanya hilo? Nitalielezea kwa undani zaidi. Jinsi alivyofanya jambo hilo, ilikuwa ... Kipeo hiki kilikuwa kimezingirwa kwa Neno, Neno la Mungu. Na kipeo, chenyewe, cha jamaa, kilikuwa kimezingirwa na Neno hili. Lakini ile sehemu iliyovunjika ilipovunjika kutoka kwa kile cha asili iliruka huo ukuta hadi ng'ambo na ikampa Shetani nafasi ya kukiharibu. Na sasa kwa kuwa mnajua kile ninachoamini juu ya mambo hayo, kwa hiyo haitanilazimu kusema jambo hilo. Lakini kile kipeo kilivunjwa.

Bali yule Mchongaji Mkuu, wakati Yeye alipoona kule kuanguka kwa familia Yake, kile kipeo, Yeye hakutaka kukiacha kimelala hapo, uso chini na katika uharibifu. Alienda kazini, mara moja, kukijenga tena. Yeye hakutaka kipotee, kilale hapo hivyo wakati wote. Kwa sababu, Yeye ni Mungu, Naye hatashindwa. Kwa hiyo, Yeye aliingia kazini mara moja na kuanza kujenga, tena, kwa mfano Wake Mwenyewe, mtu.

38 Sasa, tunaona ya kwamba ule ulimwengu uliokuwapo kabla ya gharika ulikuja ukaharibu kitu hicho chote, kwa sababu yale maagano yaliyofanywa, yalifanywa kwa masharti: "Iwapo hutafanya hili au iwapo utafanya lile." Mungu, yule Mchongaji mkuu, aliona ya kwamba mwanadamu hange—asingeweza kutimiza agano. Hawezi kufanya hivyo. Hakuna njia kamwe.

Kwenye mahojiano dakika chache zilizopita nilikuwa nikizungumza na mtu fulani chumbani, aliyepo sasa. Kasema, "Lakini, Ndugu Branham, nina mambo mengi sana ambayo ni—najua ni mabaya," na maskini mwanamke m—mcha Mungu.

Nikasema, "Lakini—lakini, angalia, dada, hujiangalii mwenyewe. Ni kile tu shauku yako na kile unachojaribu kufanya. Na kama kweli unampenda Bwana, unajaribu kumtumikia kwa moyo wako wote, na ndipo makosa yako yote yamefichwa katika Damu ya Bwana Yesu." Mnaona? Mnaona, Yeye alifanya njia.

39 Kwa hiyo akaanza sasa, akimwondoa mwanadamu katika maagano Yake, ya—ya kusema ya kwamba, "Kama ukitaka, nitafanya hivyo." Naye akaanza na mtu aliyetitwa Ibrahimu, na akampa Ibrahimu agano, bila masharti. Kila wakati angeanzisha kipeo, Shetani angekipata, kwa sababu Neno ... Lakini wakati alipoanza na Ibrahimu, Yeye alisema, "Tayari nimefanya jambo hilo." Sasa hili bila masharti, si ninii ... hilo—hilo, "Mkitaka, nitafanya," bali, "Nimefanya hivyo tayari." Sasa Yeye, yule—yule Mchongaji, amekusudia kuwa na kipeo hiki.

Ndipo, kutoka kwa Ibrahimu, wakaja wale wazee wetu. Na wale wazee kweli ... Sasa Mungu anafanya nini? Yeye anajenga tena kipeo hiki kilichoanguka. Kwa hiyo, katika wale wazee wetu, wa kwanza tunaona alikuwa ni Ibrahimu.

40 Sasa angalia, kila kipeo kimewekwa kwenye msingi, sanamu. Sanamu ya Musa ya Angelo iko kwenye kipande cha marumaru chenye urefu wa futi tatu au nne. Inao msingi. Kwa hiyo, Mungu, katika kuandaa kipeo hiki, Yeye alikiweka kwenye msingi wa wale wazee wetu. Na msingi wa mzee, kwanza, ulikuwa ni Ibrahimu, halafu Isaka, halafu Yakobo, halafu Yusufu, zile pembe nne.

Na, sasa, Ibrahimu alikuwa msingi wa imani. Hebu tuseme kilikuwa na misingi minne. Msingi wa imani ulikuwa ni Ibrahimu. Msingi wa upendo ulikuwa ni Isaka. Msingi wa neema ulikuwa ni Yakobo, neema ya Mungu kwa Yakobo; mtu yeyote anajua jambo hilo. Lakini katika Yusufu kulikuwako na ukamilifu, hapo ndipo Yeye angeweza kuweka jiwe la ukumbusho; si juu ya msingi wa kwanza, msingi wa pili, msingi wa tatu, bali juu ya msingi wa nne.

41 Ibrahimu alimdhahirisha Kristo, bila shaka; vivyo hivyo na Isaka, katika upendo. Ibrahimu alifanya hivyo, katika imani; Isaka alifanya hivyo, kwa upendo; Yakobo alifanya hivyo, kwa neema Yake. Kwa sababu, Yakobo maana yake ni "mdanganyifu," na hivyo ndivyo alivyokuwa, bali neema ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Lakini ilipofikia Yusufu, hakuna kitu dhidi yake, mkwaruzo mmoja mdogo tu, kwa maana msingi lazima pia uwe ni kipeo. Wakati alipomwambia baba yake, nabii, "Mwambie Farao ya kwamba watu wako ni—ni wafugaji wala si wachungaji, kwa sababu mchungaji ni chukizo kwa Mmisri."

Lakini wakati yule nabii mzee alipofika mbele ya Farao, yeye alisema, "Watumishi wako ni wachungaji." Kwa hiyo ikakikwaruza, mnaona, hiyo ndiyo sababu bado inakifanya kipeo.

42 Sasa misingi imewekwa, kwa njia ya imani, upendo, neema, na utimilifu, kupitia kwa wale wazee wetu.

Sasa, kiwiliwili cha kipeo hiki kikuu kilikuwa manabii, ambao walikuwa Neno. Natumaini mnaweza kulisoma. Mnaona? Manabii; si sheria! Manabii, kwa kuwa manabii walikuwa Neno lililothibitishwa linaloufanya mwili; si wale wazee wetu. Manabii, wao walikuwa ni Neno.

Hatimaye, kwa kuwa Yeye alianza kule nyuma kabisa katika siku za Musa na akaja akawafikia manabii, kwa kila mmoja. Na hatimaye, akiujenga ule mwili, ukija karibu wakati wote. Na aliye mkuu kuliko wote alikuwa ni Yohana. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema jambo hilo. "Hakuna mwanamume, aliyezaliwa na mwanamke, aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji," kwa kuwa yeye ndiye angeweza kulitambulisha Neno.

43 Kisha mwishowe kikaja kile Kichwa kikuu, Kichwa cha wote. Mwili mwingine wote ulinena habari Zake. Msingi uliwekwa na yule mzee; bali mwili ulijengwa na Neno, ambalo lilikuwa ni manabii; na huyu hapa anakuja Mkuu wa hayo yote, Yesu alikuja jukwaani. Hapo wakati hiki Kifuniko kiliwekwa juu yake, tunapata katika Yeye kazi yote ya mikono ya Mungu. Tunaona ndani Yake uakisi mkamilifu wa Neno, kwa kuwa Yeye alikuwa Neno, utimilifu wa Neno. Sasa, tena, Mungu ana Kipeo kikamilifu tena.

Kama vile Isaya alivyosema, "Tazama Mtumishi Wangu, Kipeo Changu, ambacho nimemwonyesha katika nyakati zote za Huyu aliye mkamilifu akija. Na huyu hapa amesimama moja kwa moja mbele Zangu, mkamilifu!" Hapo, katika mfano Wake Mwenyewe, akimwonyesha Mungu! Kwa maana Yeye alisema katika Yohana Mt. 14, "Mnaponiona Mimi, mnamwona Baba."

44 Na halafu, "hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu;" naye Neno

alichongwa akaonyesha jinsi Neno lilivyokuwa hapo mwanzo. Yeye, Neno, lilidhihirishwa katika Kipeo katika sura Yake Mwenyewe, Mungu alirudi tena katika mfano Wake Mwenyewe, umbo la Neno likiakisiwa katika mfano wa mwanadamu, Kipeo.

Manabii wote walikuwa na kasoro; hao wote walikuwa sehemu. Bali hapa mwishowe anakuja yule Kipeo akipitia kwao, yule Mtu mkamilifu, hamna dosari kabisa ndani Yake, mkamilifu sana, akidhihirisha alivyo yule Mjenzi Mwenyewe, Sura Yake ilidhihirishwa katika Kazi Yake. "Mungu na Kristo walikuwa Mmoja," hata Yeye akaweka Roho Wake Mwenyewe ndani Yake, na halafu hata sanamu na Mjenzi wakawa Mmoja. Mungu na kazi Yake ya uchongaji, Kipeo Chake! Ambapo Musa—Musa aliyekuwa katika kazi ya San Angelo alikuwa ... ama Michelangelo, hasa, ilikuwa ni—ni kazi ya kuchonga sanamu iliyokuwa imekufa, kwa sababu ilikuwa imetengenezwa kwa jiwe. Lakini hapa, yule Mjenzi Mkuu, wakati alipokamilisha kazi ya mikono Yake, aliingia ndani Yake.

45 Mkombozi wa mwanadamu aliyekuwa amekamilika, mkamilifu kabisa, mcha Mungu; hata hivyo, hapakuwepo na uzuri hata tumtamani Yeye. Wakati huyu Mwana wa Mungu Aliye Hai aliyezaliwa na bikira alipokuwa mkamilifu kabisa, na mnyenyekevu, na katika mfano wa Mungu, hata yule Bwana mkuu aliyekuwa amepitisha uhai Wake kwa manabii ... Naye alikuwa ni utimilifu wa manabii wote. Yeye alikuwa mkamilifu sana, hata, Mungu alipoona jambo hili, Yeye alimpiga na kulia kwa sauti kuu, "Nena!" kama vile Michelangelo alivyofanya. "Nena!"

Mnasema, "Hiyo ni kweli?"

Marko Mtakatifu 9:7, tunaona, juu ya Mlima wa Kugeuzwa Sura, wakati Musa aliposimama, ile torati, hapo alisimama Eliya, manabii. Huko nyuma kabisa kutoka kwa wale wazee wetu, baba zetu, torati, manabii, na hao wote wamesimama pale. Tunasikia Sauti ikishuka kutoka kwenye lile wingu, na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye!" Na kama watasikia, hana budi kunena. Ilikuwa ni siku chache tu kabla ya Yeye kupigwa. "Huyu ni Mwanangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake. Nimemfanyanga. Nimekuwa miaka elfu nne nikimleta kwenye jambo hili. Na sasa, Yeye ni mkamilifu sana, sina budi kumpiga Yeye apate kunena. Msikieni Yeye! Yeye ndiye aliyekamilishwa. Yeye, Yeye ni Kipeo."

46 Kumbuka, Yeye alidhihirishwa kila wakati, huko nyuma katika Agano la Kale.

Tunamwona Yeye ni Mwamba jangwani, uliopigwa, Mwamba jangwani. "Mimi Ndimi ule Mwamba uliokuwa jangwani." Lakini hilo lilikuwa ni jiwe ambalo lilikuwa halijafikia ukamilifu wake bado. Bali katika mfano Hilo lilifuata Kanisa kutoa Kwake kile ambacho Yeye angeweza kutoa, na kuwapa Uzima hao ambao Yeye angeweza kuwapa Uzima. Lakini Yeye alikuwa ndiye ule Mwamba jangwani. Hakuwa amefanywa mwanadamu bado. Yeye alikuwa katika mfano tu.

Musa alimwona amesimama juu ya Mwamba huu. Yeye alimwona akipita, naye akasema, "Ni sehemu ya nyuma ya mwanadamu." Mnaona, yule Mchongaji alikuwa akimwonyesha Musa, mfano usiodhihirika wa Kristo, jinsi kile Kipeo kikuu kitakavyoonekana wakati kitakapokamilishwa. Yeye alipitisha Hiyo ... Aliingiza —ama—ama alimwonyesha Musa awali ono la sura ya kile Kipeo. Ilikuwa ni sehemu ya nyuma ya mwanadamu, wakati kilipopita nyikani.

47 Kumbuka, Angelo angeweza tu kulia na kuipiga ile sanamu, na kusema, "Nena!"

Lakini jinsi ilivyokuwa tofauti kwa Mungu, yule Mchongaji mkuu. Wakati alipomfanya mtu katika mfano Wake Mwenyewe, mkamilifu sana hivi kwamba ilimwakisi Yeye, Mungu alinena kupitia kwa mfano wa mwanadamu, akionyesha yale angefanya. Yeye alinena kwa manabii walipokuwa katika mfano wao usiodhihirika wazi, Yeye alipokuwa akiendelea kufikia Kichwa. Lakini wakati alipokuja katika Kichwa, Yeye alikuwa sura yote ya Mungu; Alikuwa akijionyesha Mwenyewe. Ndipo, akapigwa kwa ajili yetu, sasa Yeye ni Kipeo kwetu, Karama ya Mungu, Yesu Kristo, Uzima wa Milele. Natumaini hatutasahau jambo hilo kamwe.

48 Tunapoona siku zikiwa giza, tunapoona vivuli vikiporomoka! Ninapobashiri ni mizunguko michache tu ya jua. Taifa hili limekwisha." Unajua ...

Jana, tarehe nne Julai. Je mnajua, jana, tarehe nne Julai, ambapo Thomas Jefferson alitia sahihi Ilani ya Uhuru, yeye pamoja na ile halmashauri iliyokuwa pamoja naye, na ile Kengele ya Uhuru ikalia, nasi tukatangazwa kuwa taifa huru. Kulingana na historia, hapajawahi kuwa na demokrasia wakati wowote uliopita zaidi ya miaka mia mbili. Na hiyo ilikuwa 1776, Julai nne. Nasi tumbakiza miaka kumi na moja tu. Litafaulu? La, haliwezi, mnaona. Miaka kumi na moja. Na, kama likifanya hivyo, litavunja historia yote.

49 Nasi tunaona hali ya wakati. Tunaona hali za watu. Tunaona hali ya siasa. Tunaona hali ya ulimwengu. Haiwezi kudumu. Haina budi kuzama, kama Titanic. Halina budi kuzama, kwa maana kuna kutoa nafasi yao. Taifa moja hutoa nafasi kwa lingine, wakati linapoanguka. Na ufalme huu hauna budi kuanguka, na kila ufalme mwingine, kutoa nafasi kwa ule Ufalme unaokuja, ambao hauwezi kuanguka. "Kwa maana tunaupokea Ufalme usioweza kutikiswa," kupitia sura hii kamilifu ya Mungu, Kipeo.

50 Mungu, wakati alipomwalia, alikuwa amevuviwa sana! Yeye alikuwa hivyo ... kumwona jinsi alivyoonekana, na kuona umbo la—Lake, Yeye alikuwa amevuviwa sana kwamba ingekuwa ni Kipeo kikamilifu cha Mkombozi, Yesu Mkombozi. Hivyo Mungu, ili apigwe Mwenyewe, kwa sababu ya kulipia adhabu Yake Mwenyewe, Mungu na Kristo wakawa Mmoja, kusudi Mungu aweze kupigwa katika mfano huo. Na hiyo ndiyo sababu Isaya alisema, "Tulimhesabu kuwa amepigwa na kuteswa na Mungu. Hata hivyo alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

51 Ile sanamu kamilifu, Mungu-Mwanadamu! Mungu, katika *en morphe*, alikuwa amebadilika kutoka wa Kimbinguni akawa ono, na ono hilo lilionyeshwa katika ile sanamu. Nayo ile sanamu ilipigwa ili kwamba ya Kimbinguni yapate kuonja hisia za mauti, Kipeo kikamilifu cha Mungu.

Asingeweza kufanya hivyo katika Musa. Asingeweza kufanya hivyo katika manabii; Isaya, ambaye alikuwa amekatwa kwa misumeno hata akakatwa vipande-vipande. Asingeweza kufanya hivyo katika manabii waliopigwa mawe. Asingeweza kufanya jambo hilo, kwa sababu asingeweza kulisikia; kulikuwako na sehemu Yake tu.

Lakini katika Kipeo hiki kikamilifu, Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye hangemwonyesha tu Musa; Yeye angeweza kuonyesha Utu Wake wote katika Mtu huyu, na kuonja mauti kwa ajili ya jamii yote ya binadamu. Kipeo kikamilifu cha Mungu! Mungu, aliyevuviwa sana kwa kuona, Yeye akawa Mkombozi wa nyakati zote; kuzungumza kwa ajili ya wale walio huko nyuma, ambao walikuwa hapo awali, na sasa.

Ahadi zote zilitimizwa ndani Yake. Yeye alikuwa Ukamilifu wa ukamilifu. Mifano yote ilitimizwa ndani Yake; Mkombozi wa Jamaa wetu wa karibu, katika Ruthu na Boazi; mtoa sheria wetu, kutoka Mlima Sinai; Nabii wetu, kutoka nyikani, wakati alipotoka mlimani, kama vile alivyotoka jangwani; alipokuja kutoka Umilele na akawa mwanadamu, ile sanamu kamilifu!

52 Mungu, kote kote katika wakati, akikata, kwa wale wazee wetu, na kufanya jukwaa Lake, na kuwaleta kutoka kwenye mambo mbalimbali ambayo angeweza msingi huu juu yake. Juu ya jambo hili Yeye akaanza kulijenga Neno Lake, manabii. Na halafu, hatimaye, likamjia Nabii mkamilifu, Msingi mkamilifu, ono kamilifu alilokuwa nalo Mungu.

Na sasa, kusudi hili linene, Yeye ni Neno. Na kwa Neno kunena, Yeye hana budi kuingia katika ile sanamu. Na halafu sanamu hiyo inene, haina budi kupigwa. Yeye huja katika ile sanamu, halafu apate kunena, Mkombozi mkamilifu.

Mifano yote ya Agano la Kale ilikutana Naye. Kama nilivyosema hivi majuzi, Yehova wa Agano la Kale ni Yesu wa Jipya. Ndiyo.

53 Kama vile wengi wenu, wanaume, wanawake, rika langu; tulikuwa na, kote nchini, dobi nyingi za Wachina. Wakati Wachina walipoanza kuingia, walitoka Pwani ya Magharibi, wakielekea mashariki, wakija kutoka nchi ya Mashariki, wakienda huku. Na walipofanya hivyo, walikuwa ni watu ambao hawakujua lugha yetu na njia zetu, bali walikuwa ni dobi wazuri. Nao wasingeweza kuandika tikiti ili uweze kurudisha nguo zako za kulia.

Lakini, yule Mchina, alijipatia rundo la kadi ndogo zisizo na kitu hata kidogo. Basi unapokuja kuleta nguo zako, yeye angeitwaa hii kadi na kuirarua kwa njia fulani kisha anakupa kipande kimoja, naye akakiweka kile kipande kingine. Na, sasa, ni bora kidogo kuliko tuliyonayo sasa, kwa sababu wakati unaporudi kudai kilicho chako, vipande hivyo viwili havina budi kuana. Usingeweza kuigiza kama ilikubidi kufanya. Hakuna njia ya kufanya jambo hilo. Unaweza kunakili herufi, bali hauwezi ukaigiza huo mraruo. Haina budi kuendana kabisa na kipande hicho kingine. Kwa hiyo, nguo zako chafu ulizozileta, ungeweza kuzikomboa kwa risiti hii, kwa sababu ililingana na risiti iliyoachwa

54 Na wakati Mungu, kwa manabii, na chini ya torati, alipotuhukumu kutenda dhambi; na torati haina neema, inakwambia tu wewe ni mwenye dhambi. Lakini wakati Yesu alipojitokeza jukwaani, Yeye alikuwa ni utimilifu, Yeye alikuwa ni—ni utimilifu wa kila kitu Mungu alichohidi. Yeye alikuwa mfano mkamilifu, wa kufanana wa ile ahadi. Kwa hiyo, ahadi zote za Agano la Kale zilitimizwa katika Yesu Kristo. Isingewezekana kutimizwa katika Musa. Isingewezekana kutimizwa katika ye yote wa wale wanabii, bali zilitimizwa katika kile Kipeo. Na alilingana na yote aliyosema itakuwa.

Vivyo hivyo Kanisa halina budi kulingana na kila kitu ambacho Mungu ameahidi. Lazima liwe kile kipande ambacho kiliondolewa Kwake kwa kupigwa. Kwa hiyo kama ile ya asili ni Neno, basi wale waliotolewa Kwake watakuwa Neno, wapate kulingana na ubavu Wake.

55 Kwa hiyo, yule Mchina, ungeweza kudai ... Ambapo, sheria inakuhukumu na kusema ulikuwa mchafu, nawe ulikuwa na hatia, na ingeweza kukuweka gerezeni. Bali wakati alipokuja, Yeye alikuwa Mlinganisho wake, ambaye angeweza kukutoa; na kuwarudisha, kuwa—kuwa tikiti kamili, ukombozi ambao Mungu alikuwa ameahidi kule nyuma katika bustani ya Edeni. "Uzao wako utakiponda kichwa cha nyoka. Lakini,

kisigino Chake kitakiponda—kitakiponda kichwa chake.”

56 Sasa tunaona Kipeo hiki kikamilifu ambacho Mungu alikuwa amekikamilisha. Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alikuwa yote yale yaliyoahidiwa kuwa. Yeye ndiye ahadi zote, unabii wote, kila kitu ambacho Mungu alikuwa ameahidi. “Uzao wako utakiponda kichwa cha nyoka.” Sasa, Yeye hangekiponda kwa torati, asingekiponda na manabii, bali alifanya hivyo wakati Uzao wa mwanamke ulipokuwa Kipeo, Kristo. Yeye alikuwa lile Jiwe ambalo Danieli aliona likichongwa kutoka mlimani. Yeye ndiye aliyempiga. Yeye Ndiye ambaye angeweza kuponda, kuponda kichwa cha nyoka.

Maisha Yake yalilingana, hasa, maisha ya Musa. Maisha Yake yalilingana na Daudi. Hebu tuone kama ndivyo ilivyokuwa, kama Yeye ndiye kipande kinacholingana.

57 Angalia Daudi, mfalme aliyekataliwa, juu ya watu wake mwenyewe. Alikuwa ... Siku moja alipokuwa ... Mwanawe mwenyewe aliinuka dhidi yake, naye akatenganisha na kugawanya majeshi ya Israeli. Naye alikuwa, Daudi, alifukuzwa, ama kufukuzwa na watu wake mwenyewe, kutoka kwenye kiti chake cha enzi.

Na alipokuwa akitoka, kulikuwa na mtu aliyemchukia, naye anatembea pale, akimtemea mate Daudi. Mlinzi huyo akauchomoa upanga wake, kasema, “Nitaacha kichwa cha mbwa huyo kiendeleo juu yake, amtemee mate mfalme wangu?”

Daudi alisema, “Mwache. Mungu alimwambia afanye hivyo.”

Hivi hamwoni? “Mtu mwenye huzuni, anayejua huzuni. Yeye anasimama kama Kondoo, mbele ya wakatao manyoya, bubu.” Wao ... Yeye alisema hivyo. Labda Daudi hakujua alichokuwa akisema.

Lakini yapata miaka mitano, mia sita baadaye, ama zaidi kidogo, Mwana wa Daudi alikuwa akipita katika barabara zile zile, Naye akatemewa mate. Lakini angalia yaliyotendeka wakati Daudi kutoka kwa—kutoka kwa...alipokuwa mtoro, naye ametoka uhamishoni, wakati alipo—aliporudi, mtu huyo alimsihi akimtaka amani na rehema. Hata wale waliompiga watamwona siku moja atakaporudi.

58 Nasi tunaona basi, katika Yusufu, ya kwamba Yusufu alikuwa mvulana wa kipekee, wa mwisho, sehemu ya juu ya msingi, ambapo kile kipeo kilipaswa kujengwa juu yake. Ilikuwa kuanzia imani, ukaja upendo, na tena neema; ikafikia ukamilifu. Na ilikuwa vivyo hivyo kutoka kwenye ile miguu ya kule mwanzoni, ikaendelea mbele hata ukamilifu katika Kristo. Angalia jinsi alivyoonyeshwa katika Yusufu, kilele cha msingi, aliye mkamilifu kuliko wote.

Tunaona ya kwamba Yusufu alizaliwa kwa jamaa yake. Naye alikuwa kwa mwanamke halali, kwa kweli, ambaye alikuwa mke wa Yakobo. Pia angalia, pia, ya kwamba wakati alipozaliwa, baba yake alimpenda; na ndugu zake walimchukia, bila sababu. Kwa nini walimchukia? Kwa sababu alikuwa Neno.

Mnaona msingi hasa? Mnaona jinsi kichwa cha msingi kilivyokuja? Sasa, mwangalie Kichwa cha mwili, anakuja. Sasa angalia Kichwa cha Bibi-arusi kikija. Yeye alikuwa Neno.

Nao walimchukia kwa sababu alikuwa mwonaji. Yeye aliona mambo kimbele, na akawaambia. Yalitukia. Haidhuru ilikaa muda gani, yalitokea vivyo hivyo. Na kwa kuwa wa kiroho, alitengwa na ndugu zake. Walipaswa kumpenda. Lakini wao walimchukia, kwa sababu alikuwa nabii naye alikuwa wa kiroho. Nao wakamchukia.

59 Angalia, yeye aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha; akatupwa shimoni, na akidhaniwa amekufa, bali alitolewa shimoni. Na katika wakati wake wa kujaribiwa, gerezani; mnyweshaji na m—mwokaji, tunajua ya kwamba mnyweshaji aliokolewa na mwokaji akapotea. Na katika gereza la Kristo, msalabani, mmoja aliokolewa na huyo mwingine akapotea; wezi wawili, wakosaji wawili.

Nasi tunaona alitolewa gerezani mwake, akapelekwa mkono wa kuume wa Farao; ya kwamba hakuna mtu angeweza kunena na Farao, ila kupitia kwa Yusufu. Na wakati Yusufu alipoondoka kwenye kile kiti cha enzi cha Farao, na baragumu ikalia kote Misri, ule mlipuko ulitoka na kusema, “Piga magoti, kila mtu, Yusufu anakuja!”

60 Ndivyo itakavyokuwa kwa Yesu. Jinsi alivyopendwa na Baba, na kuchukiwa na hao ndugu wa kimadhehebu, bila sababu. Yeye aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha, kama ilivyokuwa; kisha akaingizwa shimoni, akidhaniwa amekufa. Msalabani; mmoja alipotea na mwingine akaokolewa. Naye akainuliwa kutoka msalabani; na anaketi mkono wa kuume wa Mungu, katika Ukuu, Roho mkuu ambaye alikuwa amekisiwa ndani Yake. Na hakuna mtu anayeweza kuzungumza na Mungu, ila tu kupitia kwa Yesu Kristo. Wazia jambo hilo! Na wakati atakapoondoka kwenye kile Kiti cha Enzi, anaanza, “Baragumu italia, na kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri.”

Kumbuka, yeye alikuwa ni mwana wa ufanisi. Kila kitu alichofanya kilifanikiwa. Kama ilikuwa ni gereza, ama popote pale, ilikuwa mafanikio.

Na je, Yeye hajawaahidi watoto Wake ya kwamba angefanya kila kitu kitende kazi kwa manufaa. Kama ilikuwa ni ugonjwa, kifungo cha gerezani, mauti, huzuni, cho chote kile, kwamba kingewafanya kazi kwa wale waliompenda. Yeye aliahidi jambo hilo, na lazima iwe hivyo. Haina budi kuwepo. Imenenwa kwetu kwa mifano katika Yeye. Yeye alikuwa ile sanamu kamilifu ya Mungu. Sasa tunaona hapa, pia, ya kwamba atakapokuja tena ...

61 Kumbuka, Yusufu kwa ufunuo aliuokoa ulimwengu, kwa unabii wake mkuu. Ulimwengu ungekufa kama isingalikuwa kwa Yusufu.

Na ulimwengu unge—ungekufa kama haungekuwa kwa Yesu. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee.” Mungu anahifadhi Uzima.

62 Tungeendelea na kuendelea! Kwa sababu, Yeye alikuwa tu sawa na Daudi. Yeye alikuwa sawa na Musa. Yeye alikuwa sawa na Eliya. Yeye alikuwa sawa na Yusufu. Kila kitu ni mfano, kilichotabiriwa katika Agano la Kale, kililingana na huo, (ni nini?) Ikionyesha Mkombozi mkamilifu. Kwamba, tungeweza kuweka nguo zetu za kale chafu kwa dobi, kwenda kuzidai tena. Zimefuliwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Tunaweza kudai kilicho chetu. Na kila kitu ambacho alikifia, tunaweza kukidai. Kwa hiyo, Yeye alikuwa Neno kamilifu, likidhihirishwa.

63 Ilimpendeza Mungu, yule Mchongaji mkuu, kumpiga, na kufanya namna hii. Tunamwona katika Isaya hapa, kama nilivyosoma, “Sisi sote tulimheshimu, tukaelekeza uso wetu Kwake. Hakuna uzuri kwamba tunapaswa kumtamani,” kila mtu akinena habari Zake, wanamdhihakiki. Ninazungumza juu Yake sasa katika siku hii, kila mtu akimdhihakiki. Mnaona? “Tulimheshimu, tulimwona.” *Kuheshimu* maana yake ni “kuangalia.” “Tulimhesabu kuwa amepigwa na kuteswa na Mungu.” Hata hivyo, Yeye, alifanya jambo hili kwa sababu gani? “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; Alichubuliwa kwa maovu yetu.”

Sasa, tungeweza kuendelea na kuendelea na jambo hilo, lakini ninaamini mna picha ya kile ninachomaanisha sasa, Mungu akijenga Kipeo Chake.

64 Lakini hebu tuisahau ya kwamba hapo mwanzo alipopiga ubavu wa Adamu, alichukua kitu fulani kutoka ubavuni mwake.

Sasa, kupigwa kwa Kristo kulikuwa kwa kusudi fulani, apate kuchukua kutoka Kwake, mmoja, awe jamaa, Bibi-arusi; Huenda akamchukua Bibi-arusi. Kwa hiyo wakati Kipeo Chake kilipokamilika, basi ilimbidi kukipiga, kutoa kutoka Yeye; si kipande kingine, si kiumbe kingine, bali cha uumbaji ule ule.

Ndugu yangu, usifikirie vibaya jambo hili, bali fikiria kidogo. Kama Yeye alichukua kutoka Kwake, uumbaji wa asili, kumfanya Bibi-arusi kwa ajili Yake, Yeye kamwe hakuumba uumbaji mwingine. Yeye alichukua sehemu ya uumbaji wa asili. Basi, kama Yeye alikuwa ni Neno, Bibi-arusi hana budi kuwa nini? Haina budi kuwa ni Neno la asili, Mungu aliye hai katika Neno.

65 Kimberley, Afrika Kusini. Wakati mmoja nilikuwa nikiangalia almasi, jinsi zilivyotolewa kule ardhini. Nami niliwaona wamelala pale. Kama, naam, yule—yule kiongozi wa ule mtambo ama hilo shimo alikuwa mmoja wa wasimamizi wangu katika mstari wa maombi. Nami nikaona almasi, yenye thamani ya makumi ya maelfu ya dola, zikiwa zimerundikana pamoja, lakini hazikuangaza hata chini ya nuru. Nami nikamwambia msimamizi wa migodi hiyo, nikasema, “Mbona haziangazi?”

Akasema, “Bwana, bado hazijakatwa. Lazima zikatwe. Halafu, wakati zinapokatwa, basi zinaakisi nuru.” Haya basi.

Kipeo hakina budi kukatwa. Angalia, kata kwa ajili ya kitu gani? Je! Kipande hicho kimekatwa? La, la. Kipande kilichokatwa kinafanywa sindano ya santuri, nayo sindano ya santuri inawekwa juu ya—ya—rekodi ambayo ni muziki usioonekana kwa ulimwengu. Lakini sindano ndiyo inayoileta, inatoa tafsiri ya kweli ya Neno.

66 Maisha Yake yalilingana na watu wote. Ilimpendeza Mungu kumpiga. Na, sasa, kwa nini Yeye akampiga? Kwa sababu ile ile ilimbidi kumpiga Adamu.

Sasa tunamwona akipigwa, akipigwa na Mungu na kuteswa, Mwana-Kondoo mkamilifu kwa ajili ya mwenye dhambi—mwenye dhambi aliyechinjwa, Kipeo kikamilifu.

67 Sasa, kwa karibu miaka elfu mbili, Mungu amekuwa tena akimfanya Kipeo. Kwa sababu, Yeye alimpiga Adamu kupata ki- ... kipande kutoka kwake, sehemu yake, ubavu wa kumfanyia mke. Na sasa hicho Kipeo kikamilifu alichokifanya pale Kalvari, Yeye alitoa kipande kutoka Kwake. Ni Agano Jipya tu, hivyo tu. Yeye alitimiza Agano la Kale. Sasa ni Agano Jipya, sehemu nyingine ya kutimizwa. Mnaona, lile Jipya na la Kale ni mume na mke. Mnaona? Na ilichukua Jipya kuta ... La Kale kuonyesha awali lile Jipya; Kristo akaja, kile Kipeo, kutimiza hilo. Sasa Bibi-arusi Wake atatimiza kila kitu kilicho katika Agano Jipya. Kipeo kingine kiko katika kutengenezwa.

68 Kama ilivyomchukua miaka elfu nne kufanya Kipeo hiki; sasa Yeye amekuwa, kwa karibu miaka elfu

mbili akitengeneza Kipeo kingine, Bibi-arusi wa Kristo, Kipeo kingine. Katika kufanya hivyo, Yeye hufanya hivyo kwa njia Yake isiyobadilika kamwe, jinsi ile ile alivyofanya Kipeo; Neno Lake. Hivyo ndivyo anavyotengeneza Kipeo Chake, kwa sababu Yeye anaweza tu kuwa Kipeo kikamilifu wakati ni Neno kamilifu.

Uchafu wowote, takataka, miingizo, vitavunjika. "Lakini mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitavunjika kamwe." Unakumbuka, katika kukata almasi, inakupasa kuwa na chombo kamili kufanya hivyo, haiwezi kufanywa na kipande cho chote kile. Nimeona tani za hivyo visagio vikubwa vikiivunja moja kwa moja, na kuziondoa hizo tani kubwa, na kuipitisha hiyo almasi moja kwa moja. La, hakiivunji hiyo almasi. Haina budi kukatwa.

69 Sasa Yeye anafanya jambo lile lile katika njia Yake isiyobadilika. Tunaona, katika Malaki 3, Yeye alisema, "Mimi ni Mungu, wala sibatiliki." Hawezi kubadilisha njia Yake.

Sasa, kama alivyoanza katika Ibrahimu. Baada ya kuanguka kwa kipeo cha kwanza, Yeye alianza katika Ibrahimu, kwenye msingi, kujenga kipeo kingine.

Yeye alianza kwenye Siku ya Pentekoste, kujenga Kipeo kingine, ile Mbegu asili, Neno. Ulianza katika Kanisa la kwanza. Ilikuwa ni kitu gani? Ile Mbegu, Neno, Neno lililodhihirishwa, ile ahadi iliyokuwa imetolewa. Yoeli alisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono." Yale atakayofanya katika siku za mwisho, mbili, miaka elfu mbili iliyopita.

70 Angalia, na ilianza kama ya asili. Kama vile Yesu alivyosema, "Neno la Mungu ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda." Na Yeye alikuwa ndiye Mpanzi. Mbegu ilikuwa ni Neno. Na, angalia, mbegu yoyote inayokaa peke yake kamwe haifanyi kitu. Haina budi kuanguka ardhini kuleta mazao yake tena. Na Mbegu hii, Kanisa hilo kamilifu, lilianguka ardhini huko Nikea, Rumi, wakati lilipofanyika dhehebu.

Sasa, wanahistoria, kumbukeni. Na ninyi ambao mtasikia kanda hii, ichunguzeni na mwone kama hiyo si kweli. Kanisa lilikufa huko Nikea, Rumi, wakati lilipochukua mafundisho ya sharti na kanuni za imani, badala ya Neno la asili. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alikuwa ameonyesha, kwa lile Kanisa la kwanza, ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Alikuwa na Kanisa lililokamilishwa; bali Kanisa, kama mbegu nyingine zote, halina budi kuanguka ardhini na kufa. Sasa, ilianguka ardhini, na kufa, na kuharibika.

71 Mwajua, nilisoma kitabu, hapa si muda mrefu uliopita. Mtu fulani aliandika ki—kitabu, na kusema, *Mungu Mkimya*. Huenda umekisoma. Ninasahau, na—nafikiri Brumback ... La, sina, sina hakika ni nani aliyekiandika. Lakini siwezi kukumbuka. Ninacho kwenye chumba changu cha kusomea. *Mungu Aliye Kimya*, Aaisema, "Mungu, miaka elfu mbili ya Nyakati za Giza alikaa kimya, na hokusogeza mkono, na akawaangalia wafia imani waaminifu wakiingizwa kwenye matundu ya simba na kuchomwa moto na Warumi; mauaji ya kila namna; na wanawake kuvuliwa nguo zao, nywele zao ndefu zikiteketezwa, kwa kutumia lami, na kuchomwa moto." Kumbuka, nywele fupi zilianzia mara ya kwanza Rumi. Nao wanawake wa Wakristo walikuwa na nywele ndefu, kwa hiyo wao—wao waliwatumbukiza katika lami na kuwachoma moto, na kuwachoma moto, nao wakiwa uchi; wakawalisha kwa simba. Na mwandishi huyu anaendelea kusema, "Yuko wapi huyo Mungu?"

Loo, upofu wa mwanadamu, wakati mwingine! Je, haujui ya kwamba hiyo Mbegu ilipaswa kufa? Kamwe hakujaribu kuwakomboa. Walianguka chini wakaenda kwa ushindi. Walishuka kwenda chini, wakivuja damu na kufa, wakiytoa maisha yao. Kwa nini? Ilikuwa ni Mbegu. Ilibidi ianguke ardhini, kama, kwanza, Yohana 12 inavyotuambia. "Mbegu ya ngano, haina budi kuanguka ardhini na kufa hapo; wala si kufa tu, bali kuoza." Lakini madhehebu hayo hayakujua ya kwamba Uhai huo ulikuwa ungali mle ndani. Ingawa kanisa lenyewe ...

72 Kwenye lile Baraza la Nikea, la siku kumi na tano za mjadala wa wanasiasa wenye umwagaji damu, wakati hao watu mashuhuri walipoingia na kutaka kuwaingiza hawa watu mashuhuri kanisani. Nao manabii walitoka kwenye jangwa hilo kule, wakila mboga na kujivika ngozi za wanyama, manabii halisi, nao wakawatupa nje. Kwa nini? Mbegu haina budi kuanguka ardhini. Haina budi kufa.

Ilikufa katika nyakati za giza, chini ya uchafu wa giza. Walidhani ilikuwa imekwisha. Mnajua, Yohana Mtakatifu 12:24, Yesu alisema, "Mbegu ya ngano isipoanguka ardhini, inakaa peke yake." Na Kanisa la kwanza lilikuwa ni ule uzao, yule Bibi-arusi, ile Mbegu, lile Neno lililodhihirishwa, lililoanguka ardhini huko Nikea, Rumi.

73 Sikilizeni, enyi Kanisa, kote ulimwenguni ambao watasikia jambo hili. Huo hapo uchafu wako, ni hayo madhehebu. Hapo ndipo Neno liliposulubiwa, nao walikubali fundisho la sharti. Na kwa mamia na mamia ya miaka ya nyakati za giza, Nguvu na dhihirisho la Neno lilifichwa kwa ulimwengu. Ni Ukatoliki pekee uliotawala. Sote tunajua jambo hilo, kama kusoma historia. Ukatoliki tu ndio uliotawala.

Bali hu—huwezi kuificha mbegu iliyochipua, haina budi kutokea (kwa nini?) Yule Mchongaji Mkuu anaishughulikia. Yeye ataijenga tena. Kwa hiyo Yeye ... Ile Mbegu ilishuka chini, Neno.

74 Tunapomwona Mtakatifu Paulo, Petro, Yakobo, Yohana, wale wote walioliandika Neno. Nao waliandika, Neno waliloandika likawa hai, na likaishi, nalo likaishi. Na tunapoona ya kwamba lilipoanza kuiva, Yohana akaanza kuandika zile nyaraka, alitupwa katika Kisiwa cha Patimo baada ya kuchemshwa katika mafuta kwa masaa ishirini na manne. Lakini Neno halina budi kutokea. Halina budi kuandikwa. Hawakuweza kumchemsha Roho Mtakatifu kutoka kwake, kwa mafuta, kwa hiyo akaja. Kazi Yake haikuwa imemalizika. Alikufa kifo cha kawaida.

Polycarp, ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa Yohana, aliendelea na Neno. Na kutoka kwa Polycarp akaja Ireneo. Na Ireneo, mtu mkuu wa Mungu aliyeamini Injili ile ile tunayoamini, "Neno limeiva." Kanisa, likijaribu kulisonga litoke nje.

75 Hatimaye ikafikia Nikea, Rumi, na huko likaanguka ardhini, baada ya Mtakatifu Martin, naye aliuawa. Mtakatifu Martin aliamini jambo lile lile tunaloamini. Yeye alisimama vivyo hivyo; ubatizo wa Roho Mtakatifu, ubatizo wa maji katika Jina la Yesu. Yeye alisimama katika jambo lile lile tunalofanya. Naye alikuwa ni nabii, na aliamini Neno kamili la Mungu. Na hatimaye wakasulibishwa, na kuondwa ardhini, na wakawekwa pale kwa mamia ya miaka, mpaka ikaoza nje, Mbegu. Miili ya kale imeoza. Nimekuwa kule San Angelo katika yale mapango ya kuwazika hao watu na nikaona walikofia na mifupa yao ilivyovunjika na kila kitu. Hatimaye walioza mpaka mifupa yao ikaisha, bali Uhai ulikuwa ungali pale.

76 Ile punje ya ngano iliyoanguka ardhini kwenye ... kwenye Baraza la Nikea, ilianza kuchipuka tena, katika Martin Luther. Kama vile mahindi yo yote yanayochipuka, ama ngano; baada ya mbegu kuoza, uhai unachipuka. Na ikaanza kumzaa Martin Luther. Alifanya nini, jambo la kwanza? Alikataa dhehebu la Ukatoliki, akapinga ya kwamba ilikuwa ni makosa. Kwa kuwa, yeye alisema, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Ilikuwa ni kitu gani? Maisha madogo madogo yaliyosababisha shina dogo. Hao walikuwa Walutheri. Hakika haifanani na punje iliyoingia ardhini, bali Uzima huo unatoka sasa.

Kisha ukafikia ubua. Kisha kulitokea nini? Katika siku za John Wesley, alifanyaje alipoleta utakaso? Yeye alidumu na Neno. Na lilifanya nini? Waluteri tayari walikuwa wameungana na kuunda madhehebu; kwa hiyo wakati ulikuwa umewadia kwa jambo fulani kutendeka. Kipeo kinajengwa sasa. Alifanya nini? Alifanya nini? Yeye alipinga hilo kanisa la Kianglikana, lilitokea katika matengenezo kama kishada. Ni kitu gani? Ile mbegu inatoa Uhai, inakua sasa.

77 Sasa, shina halifanani na mbegu, wala kishada.

Sasa, ndugu wa Kipentekoste kote katika mataifa, nawatakeni msikilize, ndugu yangu. Kama huu ndio Ujumbe wa mwisho nitakaohubiri, Hiki ni kipeo changu. Je! Unaona wakati ngano ni ... punje ya ngano inayoanguka ardhini, wakati inapoanza kujirudia kwenye punje yake—yake tena?

Angalia maumbile. Maumbile, hasa, ni Mungu. Mungu akifanya kazi katika maumbile, ndivyo tu anavyoweza. Lakini kutoka uamsho wa Kipentekoste, kama wanavyodhania, ilikuwa Mbegu; haikuwa hivyo. Sasa angalia. Lakini kitu fulani kilitokea kama tu ile Mbegu. Sasa, tazama alivyosema Yesu katika Mathayo Mt. 24:24, ya kwamba hizo roho mbili katika siku za mwisho zitafanana sana hata ingewapoteza walio wateule kama yamkini.

78 Sasa, hilo shina halionekani kama mbegu; wala kishada hakifanani na mbegu. Lakini angalia sasa, si katika siku za Luther, bali katika siku ya mwisho.

Jambo la kwanza. Kuna wakulima wa ngano wanaoketi hapa. Kitu cha kwanza kinachotokea kwenye mbegu ya ngano, karibu ungefikiri ilikuwa ni mbegu, lakini (ni nini?) ni ganda. Inaunda kitu kidogo cha nje, kama, kushikilia mbegu. Hufanya ganda. Lakini ganda si mbegu, si zaidi ya vile kishada ama shina lilivyokuwa. Ni mbebaji tu wa uhai, punje ya ngano, basi. Yohana Mtakatifu 12, mnaona, Yesu akinena.

79 Ngano, baada ya kishada (baada ya Wesley), hutoa ganda, ambalo ni la kwanza kabisa kama punje ya kitu kingine chochote. Lile ganda ni kama nafaka. Linakuja kama nafaka wakati wote, ile iliyoingia ardhini. Na wakati linapotokea, lile shina, lina Uzima ndani yake, bali hakika si punje. Inachipua kishada, chavua, bado si punje. Na halafu linatokea ganda, nalo liko tu katika umbo la ngano, kama tu punje ya ngano, bali hata hivyo si ngano. Ni katika umbo lile lile kabisa, kikamilifu.

Wapentekoste walitokea kama tu ngano ilivyotokea. Kila mmoja anatokea kwa mwingine, akitokea kwa mwingine, bali wao ni mbebaji tu. Wanaenda kwenye dhehebu. Na hivyo ndivyo Pentekoste ilivyofanya, wakaenda kwenye dhehebu. Na Wapentekoste walifanya nini walipotoka kama tu punje? Walirudi nyuma moja kwa moja, kama katika Ufunuo 17, kwa moja ya madhehebu dada. Hivyo ndivyo hasa. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

80 Sasa angalia. Injili itatoka kupitia kwa Luther, kupitia kwa Wesley, kuingia katika Pentekoste, na katika siku za mwisho itawapoteza walio Wateule kama yamkini. Walioteuliwa! Loo, enyi ndugu wa Kipentekoste, hivi hamwezi kuona?

Ngano katika mwanzo wake wa kwanza ni kama tu mbegu, inapoanza kuumbika kama mbegu, bali ni

maganda. Iliunda madhehebu, lilifanya jambo lile lile walilofanya hapa chini katika Luther. Katika Ufunuo 17, inathibitisha jambo lile lile, la makanisa.

Sasa, ile Mbegu ya nafaka ya asili ilianguka kule Nikea, kwa kuwa ilikuwa ndiyo madhehebu ya kwanza.

Angalia hapa, Uhai uliokuwa kwenye shina, kishada, yote sasa yanaishia kwenye Mbegu. Uhai uliotoka kwenye Uzao wa asili, ulikuja kupitia katika taratibu mbalimbali (taratibu tatu mbalimbali), kisha unarudi nyuma mpaka hali Yake ya asili. Haleluya! Loo, jamani! Mimi ni mtu mwenye furaha sana ulimwenguni, ya kwamba Mungu ameniruhusu kuona jambo Hili. Angalia jinsi Neno na haya (maumbile) yanavyofanya kazi pamoja.

81 Kama tu tunavyothibitisha ufufuo; kuchomoza, kwa jua; kutua kwa jua; kuchomoza tena.

Jani likitoka mtini kuingia chini ndani ya—utomvu kuingia mzizini, na kurudi juu na—na jani linarudi pamoja na utomvu tena. Kupukutika ardhini; uhai wa huo mti hulinyonya ukalirudisha, yale madini ya chokaa na potash, na kulirudisha moja kwa moja katika jani lingine tena.

Mnaona, maumbile yote, kila kitu hufanya kazi moja kwa moja na—pamoja na Neno la Mungu. Na hii hapa, hasa, kikamilifu katika hizi Nyakati za Kanisa. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu alishuka na kuchora vitu hivyo na kutufafanulia kwa jinsi Yeye amefanya. Hiyo ni kweli kabisa.

82 Angalia, hapa, Uhai uliokuwa kwenye ganda. Katika shina, na katika kishada, katika ganda, vyote vinakusanyika katika Mbegu. Nao Uhai uliokuwa kwenye shina, ulienda, mmoja alienda kutengeneza mwingine. Kuhesabiwa haki, kulifanywa njia ya utakaso; kutakaswa, kulifanywa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu; ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulifanya njia kwa ajili ya Roho Mtakatifu Mwenyewe kushuka moja kwa moja katika ukamilifu, kurudi kwenye Neno tena, kujidhihirisha Mwenyewe.

Lakini, kile kilichounda madhehebu, kinakufa. Kama vile Uzima, katika Luther, ulienda kumfanya Wesley; na—na, kutoka kwa Wesley, ulienda kwa Pentekoste; na, kutoka Pentekoste, kufanya Mbegu asili. Na kuendelea hadi Pentekoste, inatoka kwa Wesley, mpaka wakati huo. Sababu ya Pentekoste kutoka kwa Wesley, kwa sababu haikuwa dhehebu, Pentekoste ilikuwa hivyo. Ndipo Pentekoste ikaenda kuunda madhehebu, na (ilifanya nini?) Ikageuka kuwa ganda. Ilionekana kama Kitu halisi.

83 Na, mtu ye yote, ni wangapi waliopata kuona mbegu—mbegu ya ngano ikianza kukua? Kitu kidogo cha kwanza ni nini? Ni sawa kabisa na mbegu, bali ni ganda.

Mnaona zile hatua tatu? Shina; kishada, ama chavua; halafu ganda; na halafu, kutoka kwenye ganda, inatoka ile Mbegu asili. Mnaona? Si Mbegu; ulikuwa ni Uhai wa Mbegu, ukikua kupitia huu, ukaja kwenye Mbegu. Amina, amina! Mnaona jambo hilo? Ni kitu gani? Ufufuo, ukirudi kwenye Kipeo tena, kama yule aliyeingia.

Pentekoste ilitoka kwa Wesley, kwa sababu Wesley alikuwa ni dhehebu. Pentekoste ilitokea, kama siyo dhehebu, kisha ikageuka kuwa moja. Ilibidi ifanye hivyo, kutengeneza ganda. Neno la kweli la Uzima juu yake, lilikuwa likielekea basi kwenye Punje ya asili, kupitia kwenye hatua hizi. Kupitia kwa ubua, kisha katika mbelewele; kutoka kwenye mbelewele hata kwenye ganda; na kutoka kwenye ganda, ukafanyika Mbegu.

84 La, ubua, kishada, ganda, Wakiishi, wao walitoa (katika uamsho wao wa hapo mwanzo) kitu cha kushikilia sehemu fulani ya Uhai wa ile Mbegu; lakini walipounda madhehebu, huo Uhai ukaondoka humo. Hilo linathibitishwa na historia yote. Kamwe hakuna dhehebu lililopata kufanya jambo lolote baada ya kuunda dhehebu. Lilikuwa imekufa. Hiyo ni kweli.

Angalia, Uzima huo unaendelea sasa. Unasonga mbele.

Angalia, yale waliyofanya, haya yote wamefanya, yanathibitishwa na historia jinsi hasa kanisa limekuja, lisipate kumfaa Yeye tena. Dhehebu limewekwa kwenye rafu. Kamwe hakujakuwako, katika historia yote, kanisa, baada ya kuunda dhehebu, ila lile lililokufa. Na dhehebu lilikufa na halikufufuka tena. Hamwezi kuliona? Mwanamume uliye kipofu, fungua macho yako! Maumbile na Neno vikishirikiana pamoja na kulithibitisha papa hapa ya kwamba hii ni Kweli, ya kwamba ni Kweli. Uhai huo unaacha shina, kutengeneza kishada; kutoka kwenye kishada, Hutengeneza ganda; na kutoka kwenye ganda, unaingia kwenye ile Asili tena. Angalia, kutokuwa na manufaa kwake tena.

85 Uhai huu uko dhahiri sana katika safari yake ndani ya chembe ya ngano kuliko ulivyo katika mti. Mungu aliwaita watu Wake kama mti; mnaona, uhai unashuka, katika mti, na unarudi juu tena; hushuka kwenda chini na kurudi juu; mnaona, inashuka na kurudi juu. Bali katika chembe ya ngano unapanda juu kutoka ubua asili ... kupitia katika ubua, kishada, na ganda; na kile kitu ulichopitia hufa hata hauwezi kurudi kupitia mle tena. Ni kitu gani? Haufai tena. Unaendelea kufikia ukamilifu wake.

Amina! Hivi hamwoni ni kwa nini kamwe hakutumia dhehebu? Hawezi kurudi ndani yake tena.

Limekufa. Lakini Uzima huo unapita, kutoka mmoja hadi lingine. Mnaona, wanaweka kanuni za imani, na kuingiza. “Ye yote atakayeongeza neno moja, ama kuondoa Neno moja,” mnaona, amezuiwa kutoka Hilo. Haina budi kuwa ni Mbegu ya Uzima inayosonga mbele.

86 Ninatumia hili katika mfano sasa, wa Bibi-arusi, Kipeo kinachokuja. Wakati kile Kipeo kilipoanguka, kuna Kipeo kinachoinuka. Kipeo kilianguka huko Pente- ... huko Nikea, Rumi, huko Nikea. Baada ya Nikea, Rumi, alipitia katika hatua fulani; lakini anarudi tena kwenye kile Kipeo, amekamilishwa, kwa maana Huyo ni sehemu ya Neno lililolenwa na Yeye. Yeye atakuwa na “Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi.” Halitafungamana kwa njia yo yote na shirika lo lote ama dhehebu, kitu hicho kilicholaaniwa. Limepitia katika mambo kama hayo, lakini halitakuwa humo kamwe.

87 Angalia, hiyo mbegu inachipuka, Uhai huo unakuja, si kurudi nyuma. Hakutakuwako na ufufuo tena baada ya huu. Uhai unakuja, kufikia ukamilifu wake, ufufuo.

Angalia, lile ganda lilizaa ninii—ninii ... Tazama, kapi linatoa ile Mbegu asili kutoka ndani yake. Katika Ufunuo, mlango wa 3, tunaona jambo hili.

Sasa kumbukeni, Yeye hakutolewa ndani ya kanisa lingine katika Biblia, kati ya zile Nyakati Saba za Kanisa. Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo? Yeye alipitia katika Wakati wa Kanisa, kwenda kufanya kitu kingine. Lakini, hili ndilo. Hakuna kitu kingine. Lakini yule—yule Mchongaji amerudi kwenye ukamilifu tena, Neno. Mnaona? Usirudi nyuma. Jinsi lilivyo tofauti. Ndiyo. Loo!

88 Basi angalia basi, ganda, linapotokea, linafanana tu na Punje. Lakini wakati Uhai wa Punje unapoanza kuondoka kwenye ganda, kuingia kutengeneza Nafaka (Bibi-arusi), ganda linafunguka na kufukuza ile Nafaka. Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo lilivyofanya hasa.

Katika—katika Ufunuo 3, tunaona kwamba Wakati wa Kanisa la Laodikia ulimfukuza. Sasa, mnaona, haikuwa hivyo, huko nyuma katika zile nyakati zingine, kwa sababu kulikuwa na kitu kingine bado kilichotengenezwa. Ulipita tu na kwenda katika mwingine. Nimewaambia, wakati wote, hakuna madhehebu mengine yanayokuja. Tuko mwishoni. Nao walimtoa nje kwa sababu (kwa nini?) Yeye—Yeye—Yeye ni Neno, tena. Yeye ni kama yule aliyeanguka pale. Yeye ni Fundisho lile lile lililotokea tangu mwanzo.

Na wakati Mbegu Neno Inapoanza kukua, ganda linajiondoa kwake. Uhai unaacha mengine yote upate kulifuata Hilo. Hao ni waamini wa kweli, wao hufuata huo Uhai, popote huo Uhai uendapo.

89 Kama vile katika Israeli, mfano mkamilifu, kama tungalikuwa na wakati; Nina dakika chache tu zilizosalia. Lakini katika mfano mkamilifu, hapo mwanzo, kila mahali Nguzo ya Moto ilipokwenda ilikuwa ni Uzima. Mungu alikuwa ndiye hiyo Nuru. Na sijali kama ilikuwa usiku wa manane ama kama wao walikuwa mahali pazuri palipochaguliwa, wakati hiyo Nguzo ya Moto iliposonga mbele, tarumbeta ilipigwa nao Israeli wakaondoka pamoja Nayo.

Haleluya! Na wakati baragumu ilipolia, Martin Luther akaondoka pamoja Nayo. Naye akaunda madhehebu, akafa... si yeye binafsi, ni mtu yule aliyemfuata. Kisha Mungu akaondoa ule Uhai kutoka humo, akauleta Huo, akauleta Huo katika kaburi.

Ndipo Wesley akatokea. Aliona madhehebu hayo makubwa, kwa hiyo akapiga baragumu, ya utakaso, zaidi ya Neno. Mnaona? Alipofanya hivyo, waliondoka, moja kwa moja kutoka kwa—moja kwa moja kwa Luther, wakaingia moja kwa moja katika Methodisti.

Na wakati Pentekoste walipoiona, walipiga tarumbeta, ni wakati wa kurudi kwa karama. Mnaona walichofanya? Walipiga baragumu, nao wakatoka. Ndipo wakaunda dhehebu.

Lakini, kumbukeni, baada ya ganda, hizo ni hatua tatu tunazojua, hakuna kitu kingine kilichosalia ila Punje. Ee Mungu! Na halafu hiyo Punje inatolewa nje ya hayo yote. Amina na amina! Mbegu, Neno linaanza kujumba, na Uhai unatolewa kwake... Angalia sasa, kama Bwana Arusi, hapo mwanzo, yule Bwana Arusi wa kwanza... Huyu ni Bibi-arusi anayekuja.

90 Kumbukeni, Kanisa lilianza Pentekoste, nalo lilianguka huko Nikea. Lilichipuka, si kama ile chembe halisi, la; ilikuwa sehemu ya Uhai mle ndani, lakini lilichipuka kusudi liunde madhehebu. Kisha likajitoa kwenye hayo madhehebu. Halafu basi lilifanya nini? Ndipo likaondoka, kutoka kwenye madhehebu hayo, likaingia katika madhehebu mengine, likaingia katika hatua nyingine ya Neno; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaona? Na ulipokuwa unapitia kwenye huu ubua na hatua zingine, ulizidi kuongezeka.

Kumbukeni, ile mbelewele ndogo ni zaidi, kishada kinafanana sana na Mbegu kuliko ubua ulivyo. Na ganda linafanana sana na Mbegu kuliko vile kishada kilivyokuwa. Bali Mbegu Yenyewe ni zaidi ya hilo. Mnaona? Ilikitumia hicho tu kwa usafiri katika kujisafirisha.

91 Angalia, Bibi-arusi. Kama Bibi-arusi, hapo mwanzo, alikuwa ni Neno, ama Bwana Arusi; na halafu

kama Bibi-arusi ametolewa kutoka kwa Bwana Arusi, hana budi kuwa ni Neno pia. Angalia, Bibi-arusi hana budi kuwa.

Mbona, mbona Bwana arusi anapaswa kuwa Neno lililodhihirishwa, kufanywa dhahiri? Ni kwa sababu Bibi-arusi na Bwana Arusi ni Mmoja. Yeye ni kipande kilichopigwa tu kutoka Kwake. Hicho hapo Kipeo. Alipigwa. Sema ...

Michelangelo asingeweza kuzaa hilo tena. Asingeweza kurudisha tena.

Lakini Mungu atafanya jambo hilo. Yeye atamleta huyu Bibi-arusi mdogo, ambaye amepigwa, moja kwa moja kwenye upande wa Neno la asili. Na ndiye huyo hapo, hiyo hapo Kipeo, familia imerudi tena katika bustani ya Edeni.

92 Bibi-arusi huyu atafanyaje jambo hili? Ngano hii itafanyaje jambo hili? Malaki 4 ilisema katika siku za mwisho itarudishwa, (nini?) kurudishwa kama ilivyokuwa hapo mwanzo, kuirudisha! "Nitawarudishia, asema Bwana, miaka yote iliyoliwa na tunutu, na parare, na yote yaliyoliwa na vitu hivi vingine. Nitarudisha tena." Malaki 4 ilisema Yeye atairudisha mioyo ya watu, imani ya watu iwarudie wale baba wa hapo mwanzo tena. Mnaona? Tunaona jambo hili moja kwa moja mbele zetu, Kanisa. Tuko wapi?

93 Sasa, tukifunga katika dakika chache. Ninawatakeni mwone kwa makini sana jambo fulani lililotukia hivi punde.

Malaki 4 ni kurudisha, kurudi kwenye ya asili.

Ampigwa akatolewa katika kanisa—kutoka mwili wa kanisa, akapigwa pamoja na Bwana wake kwa kusudi lile lile Yeye ni Neno. Ni kama tu vile Yusufu alivyopigwa kutoka kwa ndugu zake, kwa sababu alikuwa Neno. Naye Yesu alipigwa kutoka kwa ndugu Zake, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Kanisa limepigwa ... Bibi-arusi amepigwa kutoka kanisani, kwa sababu Yeye ni Neno. Hizo hapo hatua zako tena; moja, mbili, tatu, mnaona, hasa kabisa.

94 Neno, likiishi na likitenda kazi, Bibi-arusi wa Biblia, si bibi-arusi wa kujitengenezea; Bibi-arusi wa Biblia, aliyepigwa na kuteswa na Mungu. Hana uzuri hata tumtamani Huyo, hata hivyo tulimdhania, amepigwa na Mungu na kuteswa. Hiyo ni kweli. Anasimama peke yake. Ampigwa kutoka kwenye madhehebu yote, kulingana na Ufunuo 3. Yeye amepigwa kutoka kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia ambalo alilelewa. Mnaona? Kanisa hili lililelewa katika Wakati wa Kanisa la Laodikia; hilo ni ganda. Lakini kama hao wengine walienda ...

Hivi ninyi watu wa Kipentekoste hamwezi kuona jambo hilo, kama hilo lingine lilikuwa ni ganda na likafa? Kama hilo lingine lilikuwa ganda na likafa, kama huo ubua mwingine ulipasa ufe, kama kishada kilipaswa kufa, vivyo hivyo hilo ganda lazima life; zile hatua tatu za madhehebu.

Na kumbuka, ulisema, "Vema, sasa, kulikuwa na vishada vingi vilivyoning'inia. Kuna mengi ya *haya*." Naam. Kulikuwa na Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, Waluteri, kanisa la Kristo, mambo haya mengine yote madogo yaliyoangukia juu yake, majani na kila kitu kingine kilikuwa kimeaning'inia juu yake, bali yale ya asili yalikuwa yale matengenezo, sasa, mnaona.

95 Anasimama peke yake, kama Bwana Arusi, amekataliwa na watu, amedharauliwa na kukataliwa na makanisa. Bibi-arusi anasimama hivyo. Ni kitu gani? Ni Kipeo Chake, mnaona, ni Neno ambalo Yeye anaweza kulifanyia kazi, kulidhihirisha. Kukataa!

Kwa hiyo, ubua, kishada, na ganda, kamwe havikufanyika Mbegu, la, bali daima vinakuwa kama Mbegu.

Sasa wakati wa mavuno, Mbegu imerudi kwenye Uhai wake wa asili, imerudi kwenye Biblia. Malaki 4 ilisema ingeletwa hivyo. Loo, loo, jamani! Lazima uwe na yote! Ili iwe hivi, haina budi kuwa na Neno lote. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

96 Sasa Yeye alisema nini, katika Ufunuo 10, hilo lingetukia? Kwa nini safari ya kwenda Tucson? Kulifungua Kanisa. "Katika siku za mjumbe, za malaika wa saba, Ujumbe wa malaika wa saba, Neno lote la Mungu lingedhihirishwa. Muhuri wa yale yote yaliyoachwa na ubua, naam, na mambo yake yote, yangedhihirishwa katika wakati huu."

Je! Hivyo ndivyo Neno lilivyosema? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Halafu, tunaona jambo hilo. Basi tuko wapi, mnaona, tuko wapi? Kuna jambo moja tu, mavuno yako hapa. Yeye ameiva kabisa. Yeye yuko tayari sasa kwa ajili ya Kuja. Angalia.

97 La, halitakuwa Hilo kamwe. Katika wakati wa mavuno, Mbegu imerudi kwenye hali yake ya asili, na haina budi kuwa na Neno lote, kusudi iwe Mbegu. Na haiwezekani kuwa na nusu ya mbegu; haitakua. Mnaona? Haina budi kuwa ni Mbegu yote. Siyo kwamba idhihirishwe ... Sema, "Ninaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haleluya! Ninaamini katika kunena kwa lugha." Hiyo ni sehemu tu ya ile Mbegu, a-ha,

lakini sasa hiyo imeongezwa. Haleluya! Mnaona? Ule Uhai, siyo zile karama, ule Uhai wa hizo karama. Mnaona, mnaona ninalomaanisha? Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu.

Shina, kishada, ganda, vimekufa na vimekauka sasa. Kuna jambo moja tu ambalo yapasa litendeke kwa vitu hivi, vitakusanywa katika Baraza la Umoja wa Mkanisa Ulimwenguni vipate kuteketezwa kwa moto.

98 Neno limefanyika mwili, kama vile alivyoahidi katika Luka 17, Malaki 4, na yote, mnaona, hiyo ni kweli, Ufunuo.

Uhai wote wa kweli uliokuwa kwenye shina, kishada, na ganda, sasa unakusanyika katika ile Mbegu, uko tayari kwa ajili ya ufufuo, uko tayari kwa ajili ya mavuno. Alfa amekuwa Omega. Amina. Ya kwanza imekuwa ya mwisho; na ya mwisho ndiyo ya kwanza. Ile Mbegu, iliyoingia, imepitia katika hatua fulani na ikawa ile Mbegu tena.

Ile mbegu, iliyoanguka katika bustani ya Edeni, na ikafa pale, ikarudi. Kutoka kwenye hiyo mbegu isiyo kamilifu iliyokufa pale, ilirudi kwenye Uzao mkamilifu, Adamu wa Pili.

99 Hawa wa kwanza aliyeanguka, na akatumiwa katika yale matengenezo ya pili ... kuja kwa pili, kwa kumzaa mtoto, sasa amekuwa Bibi-arusi wa kweli tena, ile Mbegu, kurudi moja kwa moja kwa Neno asili tena.

Alfa na Omega ni sawa. "Al- ..." Yeye alisema, "Mimi ni Alfa na Omega," Yeye hakusema kitu cho chote katikati. A-ha. "Mimi ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho." Naam, bwana.

Huduma ya kwanza na huduma ya mwisho ni sawa. Ujumbe wa kwanza na Ujumbe wa pili (wa pili) ni kitu kile kile. "Mimi, nilikuwa katika Alfa; Niko katika Omega." "Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, bali wakati wa jioni itakuwa Nuru." Mnaona, Alfa na Omega, imekuwa ya kwanza na ya mwisho. Loo, jamani, ndugu, tungeweza kukaa saa nyingi kwenye jambo hilo.

100 Kipeo kikuu cha familia, Adamu wa Pili na Hawa wa Pili, sasa tayari kwa ajili ya bustani, ule Utawala wa Miaka Elfu, amina, huko nyuma duniani. Haleluya! Yule Mchongaji mkuu hakuwaacha wamelala pale. Yeye alichukua muda, kama alivyofanya kwa mamilioni ya miaka, akiwaumba wanandoa wa kwanza wakamilifu; nao wakaanguka. Sasa imekuwa katika maelfu ya miaka, Yeye ameumbika tena, na sasa hapa wako tayari.

Yule Kipeo amekuja na kupigwa; kutoka ubavuni Mwake amekuja msaidizi.

Naye amelelewa katika utaratibu ule ule. Sasa, yuko hapa tena huku maumbile yote, Biblia, na kila kitu kinginecho, vikionyesha tumefika.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara zinazotabiriwa na Biblia;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, (angalia kundi hili la takataka tulizonazo), zikiwa
zimekumbwa na hofu,
Rudini, Enyi mlidharauliwa, makwenu.

Hiyo ni kweli. Afadhali uingie humo upesi, kama unaenda.

Ninajitayarisha kufunga katika kama dakika tano, kumi.

101 Angalia kipeo kikuu, cha familia. Mume na mke hawawezi kuwa familia kweli isipokuwa wao ni mmoja. Hawana budi kuwa hivyo. Kama sivyo, wao si familia nzuri; mke anavuta upande mmoja, na mume mwingine. Hilo lingetengeneza familia mbaya sana. Lakini kwa kukubaliana, kwa upendo mmoja kwa mwingine, hiyo ni familia.

Na sasa hicho kilikuwa kipeo cha Mungu, na sasa familia yote ya kweli hapa inaonyesha hilo. Mnaona? Na sasa jamaa ya Kipeo imekuja tena, Kristo na Bibi-arusi Wake, tayari kuja. Adamu wa Pili, Hawa wa Pili, tayari sasa kurudi Nyumbani mwao. Na picha yote imekuwa ukombozi. Kutoka mahali ulipokuwa, kuirudisha, unaona, kuirudisha kabisa tena. Baada ya ...

102 Hivi majuzi, nikiwa nimesimama hapa kwa Wafanyi Biashara Wakristo. Wengi wenu, nadhani, walikuwa pale. Nilipomsikia huyo kasisi wa Kiluteri, ama mhubiri, alidhaniwa kuwa hivyo, akisimama pale na kusema lile jambo la kipuuzi, na kufanya dhahaka kwa yale tunayoamini. Na hao Wafanyi Biashara wa Injili Yote wakimweka mtu huyo pale, na kusema ya hivyo. Alivaa kola yake iliyogeuzwa. Wengi wao wanafanya hivyo sasa. Alisema, "Sasa, watu huniuliza kwa nini mimi huupindua ukosi wangu," Kasema, "Wanawezaje kukutofautisha na kasisi wa Kikatoliki." Kasema, "Hakuna tofauti, wala haipaswi kuwa." Yeye alisema, "Sisi sote tu watoto wa Mungu." Akasema, "Ninamjua kasisi wa Katoliki aliye kila mahali, mnaona, anayeweza kuwa kila mahali."

103 Sasa huwezi kuwa kila mahali bila kujua yote. Mungu hata hayuko kila mahali; Mungu anajua yote.

Yeye anajua yote, jambo ambalo linamfanya Yeye awe kila mahali, Yeye anajua mambo yote. Lakini kusudi awe kiumbe Yeye hana budi kuwa katika kiumbe kimoja. Kwa kuwa anajua yote—anjua yote, Yeye anaweza kuwa kila mahali. Maana, Yeye anajua mambo yote, na alijua kabla ya ninii ... Yeye alijua kabla ulimwengu haujaanza, ni viroboto wangapi, chawa, kunguni wangapi, na ni mara ngapi wangepumba na kufumbua macho yao, na kila kitu juu yake, mnaona, kwa maana Yeye ameenea kila mahali. Nawe huwezi kuwa mjua yote—mjua yote bila kuwa asiye na mwisho. Na kuna kitu kimoja tu kisicho na kikomo; Mungu. Amina! Na halafu sisi ...

104 Ni kitu gani? Ni ibilisi, akiwapeleka moja kwa moja machinjioni. Kila mmoja wao anaingia, jinsi hasa Biblia ilivyosema. Na hii hapa, mnaona, inakuja moja kwa moja miongoni mwa Wapentekoste, na kuwavuta tu moja kwa moja kama tu ... Ni wakati ulioje!

Loo, baada ya ushuhuda huo, mtu fulani aliniambia ... Ni—ni ... Lilikuwa ni jambo zuri ambalo sikusema sana, maana labda wangenifunga gerezeni kule. Lakini niliwazia tu, "Hilo hapo."

Wa—watu wanaofundishwa, wanajua. "Wenye hekima watamjua Mungu wao, katika siku hiyo," ilisema katika Danieli. Naam, bwana. Mnaona, "Wenye hekima watamjua Mungu wao." Wanaangalia mambo haya.

Lakini nilipoona jambo hilo likitukia, na hao Wapentekoste wakisimama pale pamoja naye! Hata Oral Roberts aliniangalia namna *hiyo*. Nikasema, "Loo, jamani!" A-ha! Bali kusimama pale na elimu, na uungwana, wajua, na kadhalika.

Hivyo sivyo Mungu anavyowaadibisha walio Wake. Yeye hawaadibishi walio Wake kwa elimu. Yeye huwaadibisha kwa unyenyekevu, katika—katika nguvu za Neno Lake lililodhihirishwa, akionyesha umbo la ile Chembe walimotoka.

105 Sasa, mtu fulani aliniambia, kasema, "Ndugu Branham," kasema, "kuna jambo moja ambalo siwezi kuelewa juu yako."

Nikasema, "Hicho ni kitu gani?"

Nikiwa nimesimama kule nje ukumbini ... Nadhani Dada Dauch na hao wengine, baada ya kupeana mkono na Bill, na nikiwa nimesimama pale na hao wote pale kwenye kona, na kundi zima la watu. Mhudumu akajipenyeza mle, ukosi uliopinduliwa, akasema, "Mbona wewe unawakemea watu kila wakati?" Akasema, "Watu hao wanaamini kuwa wewe ni mtumishi wa Mungu, uwe mpole na mzuri kwao na kila kitu." Kasema, "Kila ninapokusikia ukiinuka, unawakemea sana wanawake kwamba wana nywele fupi, na juu ya kuvaa kaptura, na kujipodoa, na mambo hayo mengine yote, na kuwakemea watu na kuwaambia jinsi walivyo baridi, watu wa kufuata desturi tu, na wasiojali." Kasema, "Kwa nini unafanya hivyo?" Kasema, "Hao watu wanakupenda. Unawezaje kuwa mwana wa Mungu mwenye upendo na kufanya jambo kama hilo?"

Nikawaza, "Bwana, hebu nimjibu mtu huyu mwerevu. Mnaona? Nijalie kumjibu kwa namna fulani ambayo itamfanya anyongwe na kamba yake mwenyewe. Naam.

Nikasema, "Vema," nikasema, "bwana, ulipata kusoma juu ya mtayarishaji mashuhuri wa muziki anayeitwa ... mtunzi mashuhuri anayeitwa Beethoven?"

Akasema, "Loo, hakika, nilisoma habari za Beethoven."

Nikasema, "Huenda ikawa alirarua vikapu kadhaa vilivyojaa makaratasi yaliyotupwa, lakini aliukabidhi ulimwengu vipeo." Kamwe hakufungua kinywa chake na kusema neno lingine. Nikasema, "Wakati alipokuwa ameketi katika chumba chake cha kusomea chini ya uvuvio, angeandika kitu fulani. Angeingia kwenye chumba chake cha kusomea na kuomba. Haukuwa sawa, angeirarua na kuitupa katika kikapu cha takataka. Bali alipopitia kwenye uvuvio wote, ulimwengu ukapata kipeo."

Loo, jinsi Neno linavyokata, bali hutoa vipeo, huondoa makapi yote pamoja na ubua. Linatoa Kipeo.

106 Nina dakika saba za kuwaambieni jambo lililotendeka juzi, tupate kuondoka katika wakati uliopangwa. Tarehe tatu Julai, nilikuwa humu nikikaa ... sokoni upande huu, madukani, upande ule kutoka hapa tulipo. Nimekuwa Pig Alley, kule Rumi, kule Ufaransa, na nimekuwa katika Jiji la New York, Los Angeles. Lakini kundi la wanawake wachafu sana niliopata kuwaona maishani mwangu ni Jeffersonville, Indiana. Sijapata kuona upotovu mwingi hivi pamoja na uchafu maishani mwangu kama ninavyouona katika hao watu. Niliketi pale hata moyo wangu ukauma, na Bwana alikuwa amenipa ono.

Sasa nitawaambia hilo ono. Sijui kama naweza kulifasiri, lakini ni—nitalisema hilo ono kwa mara yangu ya kwanza.

107 Nilipatwa na njozi. Na iliponitokea hivyo, Mtu fulani alikuwa pamoja na mimi. Sikumwona huyo Mtu. Ilikuwa ni Sauti tu. Na nika—nikaangalia. Na ni—nilipoangalia upande huu, Yeye akasema, "Bibi-arusi

atajitokeza apate kuonekana kimbele apate kukaguliwa.”

Kisha nikatazama wakijnjia, nami nikaona kundi la wanawake walio—walio wazuri mno waliovalia mavazi nadhifu sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Lakini kila mmoja wao, alionekana kama kwamba, alikuwa amevalia tofauti. Wote walikuwa na nywele ndefu. Nao walikuwa na nguo zenye mikono mirefu na marinda marefu na kadhalika. Wanawake vijana, walionekana kama, ningesema, yapata umri wa miaka ishirini.

Sasa ninayo Biblia iliyofunguliwa hapa mbele zangu. Mnaona? Ninaweza tu kusema yale niliyoona.

Kama ukisema, “Unaangalia nini?” Ninaangalia saa. “Unatafuta nini?” Ninawatafuta watu, nikiwaangalia watu. “Unaangalia nini?” Ninaangalia Biblia. Hivyo ndivyo ilivyo. Ninasema Kweli. Hivyo ndivyo ninavyoona. Nami ninaweza tu kusema yale niliyoona. Si—sijui ni ninii ... yote kuhusu jambo hilo. Inanibidi tu kuwaambia.

108 Lakini, wakati Bibi-arusi huyu, Yeye alikuwa akiangalia moja kwa moja kwenye ... Yule aliyekuwa anazungumza nami, nami, tukisimama pamoja. Macho yake, Walikuwa watu walio wasafi sana na wazuri sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Inaonekana kana kwamba ingekuwa dazani moja, ama zaidi, tu ... Sijui ni wangapi walikuwa sambamba, lakini walikuwa tu kundi. Na Yeye akapita, kwa madaha, na hewa. Na macho Yake yameinuliwa juu, akiangalia, alipokuwa akipita. Loo, Yeye alikuwa mzuri! Nikamwangalia, Naye alipokuwa akipita. Yeye alisema, “Sasa tutakagua ...” Kasema, “Huyo ni Bibi-arusi.”

“Sasa tutayakagua makanisa.” Nao wakaja. Niliwaona wakija. Na wakati walipokuja, kila mmoja, alionekana kama, alizidi kuwa mbaya. Sijapata kuona kundi chafu namna hiyo maishani mwangu.

Na wakati aliposema, “Linalofuata,” nilisikia kelele. Naye aliposema, “Linalofuata,” kasema, “hapa linakuja kundi la Amerika.”

109 Naam, mimi ni Mwamerika, lakini hili—hili lilinifanya nichefuke moyoni. Mimi sina ufasaha wa maneno wa kutosha, katika wasikizi waliochanganyikana, kusema yale yaliyokuwa yakitendeka. Ni—ni—ni ... Na itakubidi kusoma katikati ya mistari. Lakini wakati wanawake walipokuwa wakija, kiongozi wao alikuwa ni mchawi. Alikuwa na pua ndefu na mdomo mkubwa mno. Na hao wote walikuwa wamevalia kitu kama nguo za sehemu ya chini huku, bali upande wa juu ulikuwa na ukanda tu ambao, mdogo, ukanda kama wa nusu inchi uliofungiwa juu na ukawazunguka *hivi*. Na kila mwanamke alikuwa na kitu fulani kwa utaratibu ...

Wengi wenu, miaka kadha wa kadha iliyopita mlikuwa, mnakumbuka, wakati tulipokuwa tunakata hiyo karatasi, mnajua, gazeti, kutengeneza fungu la matamvua ya kale? Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo? Mnajua. Mbona, nafikiri wanalitumia katika karamu, mwajua. Vikining'inia hivyo, karatasi yenye matamvua, karatasi ya nyuzinyuzi.

Walikuwa na kitu kimeshikilia sehemu zao za chini hivi, kimeshikilia upande wa chini. Sehemu *hii* yote ilikuwa uchi.

Na kila mmoja wao alikuwa amekatwa nywele zikawa fupi sana, zimesokotwa kote, nywele zilizokatwa zikawa fupi sana, nao wamejipodoa kwelikweli. Hakika kabisa ila walionekana kama makahaba wa mitaani.

Nao walikuwa wakitembea na hii karatasi, na, utovu wa adabu! Sasa, karatasi ndiyo ilishikiliwa mbele zao. Bali walipopitia jukwaa la kukagulia, nyuma yao... Na kuona jinsi walivyokuwa wakitembea kwa sehemu zao za mbele na za nyuma, na jinsi walivyokuwa wakitenda...

Nikasema, “Hilo ni Kanisa?”

110 Nalo likapita. Nao walikuwa wakiimba nyimbo hizi za twisti na rumba, mwajua, ama cho chote mnachoziiita, huku wakiteremka, kama wanaoimba, wakienda.

Nikasema, “Hilo ni Kanisa?” Nami nilikuwa nimesimama pale, na moyoni mwangu nilikuwa nikilia.

Na, mchawi huyu, kwa maoni yangu si kitu kingine ulimwenguni ila yeye ni ... Yeye ndiye lile Baraza la Makanisa Ulimwenguni, akiwaongoza moja kwa moja barabarani walikokuwa wakienda. Walienda kushoto, nao wakatoweka katika machafuko; wangali wanapiga muziki huu na kutoa sauti za ajabu sana, na kuitikisa miili yao, upande mmoja na halafu upande mwingine. Halafu basi, namna hiyo, wakiendelea kufanya hivyo, wakitembea.

111 Nami nikaanza tu kuinamisha kichwa changu, Naye akasema, “Ngoja, lazima Bibi-arusi aje tena.”

Nami nikaangalia, na hawa hapa wanakuja tena. Nao wakupita, maskini wanawake warembo. Wote walikuwa wakiniangalia moja kwa moja, walipokuwa wakipita. Nami nikaona kila mmoja alikuwa amevaa tofauti. Na mmoja huko nyuma alikuwa na nywele ndefu zilizing'inia chini, na alikuwa amekunja namna *hii*; huenda alikuwa ni Mjerumani ama kitu kama hicho. Nami niliwaangalia.

Kisha, walipoanza kuondoka, wawili ama watatu wao huko nyuma basi wakaacha kwenda kwa utaratibu, nami nilikuwa niwakemee, Nao wakawa wanajaribu kupiga hatua kwa utaratibu tena. Nami niliwaona, lile ono tu linafifia na kubadilika, kutoka kwangu.

112 Sasa hii hapa tafsiri yake. Sababu ... Sasa, kumbukeni, nilikuwa nimemaliza tu kuandika ... Sikuwa nimemaliza, sikuwa nimeandika maandishi haya bado. Bali katika kuhubiri asubuhi ya leo, nilipata tafsiri yake katika mahubiri yangu. Je, mliona, kanisa lilionekana tu...

Sasa, hiyo ni Kweli, enyi marafiki. Baba wa Mbinguni, Ambaye huliandika Neno, anajua ya kwamba nasema Kweli. Mnaona? Ninajua ninasema tu Kweli.

Na bila kujua jambo hilo mpaka dakika chache tu zilizopita, ilionekana kama, ama hivi majuzi tu, mnaona. Mliona? Ile Mbegu ya kwanza na Mbegu ya pili, zote mbili ni kitu kile kile hasa. Na sababu ya kuvalia ... kuvaa mavazi ya namna mbalimbali, yeye atatoka katika mataifa yote, kumkamilisha Bibi-arusi. Kila mmoja alikuwa na nywele ndefu, wala hana vipodozi, na wasichana wazuri sana. Nao walikuwa wakiniangalia. Hiyo ilimwakilisha Bibi-arusi akitoka katika mataifa yote. Mnaona? Yeye, kila mmoja aliwakilisha taifa, walipokuwa wakitembea kikamilifu kulingana na Neno. Mnaona?

113 Na, basi, sina budi kumwangalia. Atakosa kupiga hatua kwa utaratibu wa hilo Neno nisipomwangalia, wakati anapopita, kama atanikaribia. Labda itakuwa wakati wakati wangu utakapokwisha, mnaona, nitakapomaliza mwendo, ama cho chote kile.

Nini? Walikuwa wakirudi. Wakijitahidi wawezavyo, walikuwa wanarudi, walikuwa wakiingia mstarini, maana walikuwa—walikuwa wakiangalia mahali pengine, wakiliangalia hilo kanisa lililoingia katika machafuko matupu. Lakini wawili ... Wale wa mbele, kamwe. Wale waliokuwa huko nyuma, wawili tu ama watatu wao, walitoka nje kidogo upande wa kulia, na ilionekana kama kwamba walikuwa wakijaribu kurudi mstarini walipokuwa wanapita. Walikuwa wakinipita, loo, kwa umbali wa kutoka hapa mpaka ukutani, wakinipita. Nami nilikuwa nimesimama pale. Kisha nikawaona wote wakitoka nje na kuondoka.

Lakini, mnaona, kanisa lilijitokeza mara moja tu, kila taifa, kanisa. Lakini Bibi-arusi aliingia mara mbili. Mnaona, mnaona ilikuwa ni nini? Sasa, bila kujua jambo hilo, bali liangalie kwa Ujumbe wangu asubuhi ya leo. Bila kujua jambo hilo. Mnaona?

114 Mbegu hiyo ilianguka ardhini huko Nikea. Huo ulikuwa ndio Uzao wa asili. Naye amepitia katika utaratibu wa madhehebu haya, ambayo yanatokea tu mara moja. Lakini Bibi-arusi atarudi tena katika siku za mwisho. "Nitarudisha." Mnaona, kile Kipeo kinaletwa. Hiyo ndiyo sababu alikuwa anaonekana, akachunguzwa, mara ya pili. Alichunguzwa mara ya kwanza, kisha akahakikiwa mara ya pili. Naye alikuwa kikamilifu, mara ya pili, kama alivyokuwa mara ya kwanza. Ee Mungu, turehemu! Haraka, haraka, haraka, Uzima, ingia kwenye Punje, upesi sana! A-ha.

115 Wengine wote hawakutokea tena. Walitoka, bila kurudi tena.

Lakini Bibi-arusi alirudi, kwa maana alikuwa ni Alfa na Omega. Mungu, yule Mchongaji mkuu, amefanya Kipeo, kwa maana ni kipande cha Kipeo Chake cha kwanza. Kama vile alivyofanya katika bustani ya Edeni, na kuchukua kipande kutoka, na kutengeneza kipande kingine na ambacho kiliharibiwa na kuanguka, sasa amekuwa katika wakati huu wote akikijenga tena. Naye akaleta Kipeo hiki, na akapigwa, katika utaratibu ... Sehemu hiyo ambayo ilikuwa imepigwa, ilikuwa ni kwa ajili ya kurudisha tena kile Kipeo, tena.

Kwa hiyo, Kipeo na Mwana wa Mungu, Kipeo na Bibi-arusi, na ni kipande Chake, ambacho hakina budi kuwa ni kutimizwa kwa Neno. Neno limetimizwa, nasi tuko tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana.

116 Enyi Kanisa la Mungu aliye hai, inamisheni mioyo yenu na wenye— wenyewe mbele za Mungu. Mambo haya ni kweli. Najua ya kwamba inasikika kana kwamba, kitu kikuu kama hicho kingekuwa, kingesambazwa kote katika mataifa. Haikuwa hivyo kamwe. Yeye habadilishi njia Yake. Iweni tu na shukrani, enyi Kanisa, shukrani kwamba mko mahali mlipo leo kama mko katika Kristo. Kwa sababu, mnaona, sasa, na wakati hilo ...

Kumbuka, Uhai huo wote utakusanywa moja kwa moja kwenye Punje, kwa ajili ya ufufuo, bali shina halina budi kuchomwa moto. Mengine; ganda na mengine yote lazima kuangamizwa, na yataangamizwa. Msiyaamini madhehebu yenu, hayo. Wewe dumu katika Neno, Uzima, Mungu na Kipeo Chake.

Basi ni kitu gani katika ule Utawala wa Miaka Eflu? Kristo na Bibi-arusi Wake, huko nyuma katika bustani ya ule Utawala wa Miaka Eflu. Amina!

Nampenda, nampenda
Sababu alinipenda
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

117 Hapo ndipo alipopigwa. "Tulimhesabu kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu."

Je! Kuna yeyote hapa, asubuhi ya leo, ambaye hayuko katika hiyo Nafaka asubuhi ya leo? Na kwa kuwa Uhai sasa unavuta kipande chake cha mwisho kutoka kwenye ganda, kwa kuwa ganda linakauka. Ni wangapi wanaojua ya kwamba kanisa la Kipentekoste linakauka? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ni kitu gani? Uhai unaliacha. Kwa kweli, limeachwa. Na iwapo huyo Bibi-arusi tayari ameonekana kimbele, nashangaa basi kama Bibi-arusi tayari hajafanyizwa. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, Nampenda.]

... mpenda, nampenda
Sababu alinipenda
Akanunua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

118 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa. Kuna wengine hapa ambao wangetaka kukumbukwa? Kama ukijisikia ya kwamba wewe si ...

Marafiki, ni dhahiri sana. Sijawahi kupata ono maishani mwangu, isipokuwa kitu fulani kitokee, kifuatwe. Ninasema Kweli. Nyakati hizi zingine zote, kama nimesema Kweli, Mungu amelithibitisha. Halafu, ninasema Kweli wakati huu.

Sijui tunaishi katika siku gani, bali ninajua hakuna kitu kilichosalia. Kusingekuwako na mwanasiasa anayeinuka ambaye angeweza kunyoosha jambo hili. Siasa, taifa limekwisha. Ee Mungu! Mnaweza, mnaweza kuingia ndani kabisa vya kutosha ku—ku—kuhisi jambo hilo. Taifa limekwisha; si taifa, bali mataifa. Hili ndilo kundi bora kuliko lote, na limekwisha. Halafu, kama mataifa yamekwisha, ulimwengu umekwisha. Na makanisa, kwa maoni yangu, Pentekoste ndiyo iliyo bora sana waliyokuwa nayo, bali imekwisha.

Ee Mungu, turehemu!

119 Kama humjui, tafadhali fanya haraka, harakisha. Kama ukijisikia Uzima, toka kwenye ... toka kwenye dhambi yako, toka kwenye kitu ulicho ndani yake. Kama ukihisi ule Uzima, ondoka katika ... ondoka katika dhambi yako, ondoka kwenye kitu ulichomo. Ingia kwenye ile Chembe haraka. Utakufa katika shina, ama kwenye ganda.

Ombeni, tunapimba sasa. "Nampenda."

Ni juu yako sasa. Hatuna madhehebu, wala chochote. Tuna Kristo tu. Mnakaribishwa kuabudu pamoja Naye, pamoja nasi, mpaka Yeye atakapokuja. Hatuwezi kuandika jina lako kwenye kitabu; hatuna vitabu. Tunataka jina lako katika Kitabu cha Uzima. Unaweza tu kufanya hivyo kwa Kuzaliwa. Hivi hutafanya hivyo sasa hivi? Mwombe Kristo apate Uzima mpya, akulete, aandike jina lako kwenye Kitabu Chake, kama sivyo. Basi, unaweza kushiriki pamoja nasi, tungependa kuwa nawe. "Mimi ..."

120 Mungu mpenzi, msaidie kila mtu sasa kuchukua hesabu, angalia kama tuko ndani Yake. Ulitupenda. Ulipigwa kwa ajili yetu, nasi tulidhania ulipigwa na kuteswa na Mungu. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamwita kila mmoja. Bwana, nena na watoto wangu, wapendwa wangu, marafiki zangu. Tujalie, Bwana, sasa hivi, kupitia Jina la Yesu Kristo.

Usimwache mtu yeyote asubiri kwa muda mrefu sana, Bwana. Inaonekana karibu sana. Mavuno kweli yameiva. Chombo cha Mungu cha kuvuna kitapitia nchini mbio katika mojawapo ya siku hizi; majani makavu yatarushwa kila upande; bali Ngano itakusanywa ghalani, itwaliwe, kwa sababu katika Hiyo kuna Uzima. Jalia, Bwana, kila ombi lijibiwe, kila ombi lidhihirishwe mbele Zako.

Ninawaomba, Bwana. Ninaomba ya kwamba hutamwacha yeyote aliye hapa apotee, Bwana. Wao—wao—wao wanaketi chini ya magumu; wao—wao—wao huendesha gari kwa mamia ya maili. Na cho chote tunachohitaji, tupe, Bwana, cho chote kinachotufaa, Bwana; si yaliyo mema machoni petu, bali yaliyo mema machoni Pako. Tunataka kusimama kama bikira safi aliyekaripiwa, kukemewa na Mungu, tupate kusafishwa dhambi zetu. Nami ninatoa ombi langu kwa ajili yao, Bwana.

121 Si—si—sijui jinsi ya kuomba. Tu—tunazungumza na Mungu Mwenye Nguvu. Na ni mwanadamu yupi aliyepo, ni binadamu gani awezaye kufanya ombi linalofaa mbele za Mungu Aliye Hai? Lakini, Bwana, maneno yangu yasiyotamkwa vizuri na—na majina yangu ya vitu na vijina ka—katika mahali pasipofaa, kama Wewe ungaliweza kutambua A-B-C za mvulana mdogo siku moja na kutunga sentensi, Wewe—Wewe waweza kuacha majina yangu ya vitu na vijina na uangalie tu yale ninayoamini, Bwana.

Ninakuamini. Ninaamini Neno hili. Nami ninaamini kwa ajili ya kila mmoja hapa. Nami ni—ninawaleta kwenye Madhabahu hiyo, Bwana, kwa imani, ambapo kati yetu na Yehova Mkuu kuna Damu ya Mwanawe, Yesu. Nayo Damu itanena kwa niaba yetu. Wakati ulipompiga pale Kalvari, Wewe ulisema, "Nena!" "Msikieni Yeye!" Na hiyo Damu, Biblia ilisema, inanena mambo makuu kuliko damu ya mwana-kondoo katika Agano la Kale; kwa kuwa Damu ya Kristo inanena makuu kuliko damu ya Habili, mambo

makuu zaidi. Nawe nena, Bwana, ukombozi kwa ajili yetu, tunapokuita kupitia ile Damu.

122 Baba Mkuu wa Uzima, tujumuishe sisi, Bwana. Kama sisi—kama tumefanya dhambi, tuondoe. Sisi, hatutaki kuwa hivyo, Bwana. Si kusudi letu.

Nasi tunatambua ya kwamba tunaishi katika njia yenye giza la kutisha. Kama tulivyosema hapo mwanzo, tunapanda mlimani, kupitia sehemu zilizoparuzika. Mkondo wenye utusitusi; bali tunabeba Taa. Jalia tuione Njia hatua kwa hatua tunapotembea sasa, hata tutakapokutana, kama *Safari ya Msafiri*, hata mwishowe tutakapofika juu ya kile kilima. Tuongoze, Ee Mchungaji. Yehova mkuu, tuongoze kwa Roho Wako.

Nasi tunajua ya kwamba tuko mbali na kipeo, lakini tunaangalia tulikotolewa, kile Kipeo halisi, nasi tunamtumainia Yeye. Tupeleke tu Kwake, Bwana. Tujalie, Bwana.

123 Waponye wagonjwa wote hapa, Bwana. "Tulidhania kuwa amepigwa na kuteswa. Bali Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu." Kipeo cha Mungu kilipigwa. "Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Waponye wagonjwa, Bwana, katika Uwepo Wako wa Kiungu sasa, huku tukijua ya kwamba Wewe upo hapa.

Safisha nafsi zetu, mioyo yetu, na maovu yote, mawazo yote mabaya, mawasiliano yote mabaya, mambo yote yaliyo mabaya. Tusafishe. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utaponya magonjwa yetu, na hebu tuondoke hapa tukijisikia ya kwamba sisi ni watoto Wako waliotakaswa. Na huku Damu ikiwa juu yetu, tunanena kwa Damu, Neno. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

124 Baba Mungu, juu ya lesa hizi, zipake mafuta kwa Uwepo Wako, Bwana. Jalia Uwepo Wako uwe pamoja nao popote waendapo. Po pote zitakapowekwa, juu ya mwili wo wote mgonjwa, jalia waponywe. Na cho chote kile, kama kuna nyumba iliyovunjika mahali fulani, itengeneze, Bwana, yule Mchungaji mashuhuri. Tujalie, Bwana.

Tufinyange, na utufanye wana na binti za Mungu. Tunaamini ya kwamba Bibi-arusi anafanyiwa matayarisho ya mwisho. Atapigwa atolewe kutoka katika dhehebu nzima kwa jumla, na ndipo yale mavuno makuu yatakapokuwepo hapa. Mpaka wakati huo, Bwana, uwafanye wenye afya na wenye furaha, kukutumikia. Katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, na- (kweli mnampenda?)
Sababu alinipenda
Akanunua wokovu wangu
Kwenye ...

125 Sasa mnaelewa ni kwa nini ninawakemea? Hiyo si kwa sababu ninawapenda ... si kwa sababu siwapendi. Ninawapenda. Ninataka Kito cha Bwana. Huenda ikanilazimu kurarua wachache na namna hii, bali nitapata Kipeo mojawapo ya siku hizi nikikiweka moja kwa moja katika Neno hili. Sawa.

Sasa Yesu alisema, "Watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Tunapaswa kupendana sana sisi kwa sisi!

Kibarikiwe kifungo kinachofunga
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ile nia ya ushirika wa kindugu
Ni kama ile ya Juu.

Hebu na tupeane mikono.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaunganishwa moyoni,
Nami ninatumaini kukutana tena.
Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na shida;
Litakuwa furaha na faraja,
Popote uendapo.
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa kumbuka, katika safari yako:

Peleka Jina la Yesu,
Akiwa ngao kutoka kwa kila mtego;
Wakati majaribu yanapokukusanyikia ... (Unafanya nini basi?) ...
Pumua tu Jina hilo katika maombi.

Ee Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Mpaka tuonane!

Na tuinamishe vichwa vyetu. Loo, napenda kuimba!
Hata tutakapokutana miguuni pa Yesu;
Hata tuonane! hata tuonane!!
Mungu awe pamoja nanyi!



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7